IJA - WORKERS SACCOS LTD.

Reg. No. TAR 526, P.O.Box 20, Lushoto - Tanga, Tel:+255 (0) 272640133,

Fax: +255 (0)272640287, E-mail: ijaworkerssaccos@gmail.com

MWONGOZOUSIMAMIZIWAVITAHATARISHI

Imeandaliwana:

BODI IJA WORKERS SACCOS LTD,

S.L.P 20,

LUSHOTO.

TOLEOLAKWANZA DECEMBER, 2024

CamScanner

YALIYOMO

YALIYOMO
DIBAJI ..... i-iv
SURAYAKWANZA v
UTANGULIZIWAMWONGOZOWAUSIMAMIZIWAVIHATARISHI 1
1.1 Utangulizi 1
1.2 LengolaMwongozo 1
1.3 UfafanuziwaVihatarishikatikaVyamavyaUshirikawaKifedha 1
1.4 MpangowaUsimamiziwaVihatarishi 2
1.5 UsimamiziwaVihatarishi 3
1.6 MamboMuhimuyaKuzingatiakatikaUandaajiwaMuundowaUsimamiziwaVihatarishi 3
1.6.1 BodinaMenejimentikatikausimamizi wachama.4 5
1.6.2 Sera,kanuni,taratibunaukomo/mipaka 6
1.6.3 Upimajitoshelevuwavihatarishi,ufuatiliajinamfumowausimamiziwataarifa 7
1.6.4 Mfumothabitiwaudhibitiwa ndani 7
1.6.5 Mapitiohuruyamfumowausimamiziwavihatarishi 8
1.6.6 Mfumojumuishiwausimamiziwavihatarishi 8
1.6.7 Mpangowadharurajuuyavihatarishi 9
SEHEMUYAPILI 10
USIMAMIZIWAKIHATARISHICHAMIKOPO 10
2.1 Utangulizi 10
2.2 WajibuwaBodinaMenejimentikatikaKusimamiaVihatarishi 10
2.2.1 Wajibuwabodi 10
2.2.2 Kamatiyamikopo 11
2.2.3 Menejimenti 11
2.3 MkakatiwaUanzishajinaUendelezajiwaBidhaa 12
2.4 Sera,TaratibunaMipaka/Ukomo 14
2.4.1 SerayaMikopo 15
2.4.2 Mgawanyowamajukumu 16
2.4.3 Bidhaaza mikopo 17
2.4.4 Utaratibuwautoajiwamikopo 18
2.4.5 Ufuatiliajiwawakopaji 18
2.4.6 Dhamanayamikopo 19
2.4.7 Mfumowandaniwaupimajiwa vihatarishi 20
2.4.8 Usimamiziwamikopomibaya 21

CamScanner

2.4.9 Miamalakatiyachamanataasisinyinginezakifedha 22
2.4.10 Matengonataratibuzakufutamikopomibaya 22
2.5 UpimajinaUfuatiliajiwaVihatarishivyaMikopo 22
2.5.1 Upimajiwavihatarishivyamikopo 22
2.5.2 UsimamiziwaMikopo 23
2.5.3 UtoajiwaTaarifazaVihatarishi 24
2.5.4 Mfumowausimamiziwataarifa 25
2.6 UdhibitiwaNdanina Ukaguzi 26
SEHEMUYATATU 27
KIHATARISHICHAMKAKATI 27
3.1 Utangulizi 27
3.2 VyanzovyaUjumlavyaVihatarishivya Kimkakati 27
3.3 WajibuwaBodina Menejimenti 27
3.3.1 WajibuwaBodikatikakudhibiti Vihatarishi 28
3.3.2 Wajibuwamenejimenti 28
3.4 Sera,TaratibunaUkomo 28
3.4.1 Mchakatowampangomkakati 28
3.4.2 Mamboyakuzingatiakatikauandaajiwampangomkakati 29
3.5 MamboyaMsingiYanayotakiwaKuwemokwenyeMpangoMkakati 30
3.6 MpangiliowaMabadilikokatikaMenejimenti 31
3.7 MichakatomingineyaKusaidia 31
3.7.1 Mpangowausimamiziwamahitajiyafedha 31
3.7.2 UsimamiziwamifumoyaTehama 31
3.7.3 UsimamizinamaendeleoyaRasilimaliWatu 32
3.7.4 Mpangowaurithishaji(*successionplanning*) 33
3.8 Upimajina Ufuatiliaji 35
3.9 UdhibitiwandaninaUkaguzi 36
SEHEMUYANNE 37
USIMAMIZIWAKIHATARISHICHAUENDESHAJI 37
4.1 Utangulizi 37
4.2 WajibuwaBodinaMenejimenti 37
4.2.1 WajibuwaBodi 37
4.2.2 WajibuwaMenejimenti 38
4.3 SeranaUtaratibuwaUsimamiziwaVihatarishivyaUendeshaji 38
4.4 Upimaji,UfuatiliajinaUdhibitiwaVihatarishi 39
4.4.1 Upimaji 39
4.4.2 Ufuatiliaji 39

CamScanner

4.4.3 Udhibitinakukabiliananavihatarishi 40
4.5 Udhibitiwandaninaukaguzi 41
SEHEMUYATANO 42
USIMAMIZIWAVIHATARISHIVYATEKNOLOJIAYAHABARINAMAWASILIANO 42
5.1 Utangulizi 42
5.2 WajibuwaBodina Menejimenti 42
5.2.1 WajibuwaBodi 42
5.2.2 WajibuwaMenejimenti 43
5.2.3 MkuuwaidarayaTeknolojiayaHabarina Mawasiliano 43
5.2.4 Mchakatowaajiraza Watendaji 44
5.3 MkakatiwaTeknolojiayaHabarinaMawasiliano 44
5.4 MiundombinuyaTeknolojiayaHabarinaMawasiliano 44
5.5 SeranaTaratibuzaUsimamiziwaTeknolojiayaHabarinaMawasiliano 45
5.6 UtambuziwaVihatarishi 45
5.7 Tathmini,UpimajinaUfuatiliajiwaVihatarishi 45
5.7.1 Upimajiwavihatarishi 46
5.7.2 Uzuiajiwavihatarishi 46
5.8 UdhibitinaUkaguziwa Ndani 47
5.8.1 Ukaguziwandani 47
5.8.2 Mawandayaukaguziwandaniwa TEHAMA 47
5.8.3 Jukumulaukaguziwandanikatikautekelezajiwamfumompya 47
SEHEMUYASITA 48
UDHIBITIWAKIHATARISHICHAUKWASI 48
6.1 Utangulizi 48
6.2 WajibuwaBodinaMenejimentikatikakudhibitikihatarishichaUkwasi 48
6.2.1 WajibuwaBodi 48
6.2.2 WajibuwaMenejimentiyachama 49
6.2.3 KamatiyaMalinaMadeni/dhimazachama 49
6.3 SeranaTaratibuzaUsimamizi 50
6.4 UpimajiwaVihatarishivyaUkwasi 50
6.4.1 Takwalakisherialakiwangochachinichaukwasiwachama 50
6.4.2 Uwianomwinginewaukwasi 50
6.5 Ufuatiliajiwaukwasi(*LiquidityMonitoring*) 51
6.6 MpangowaDharurawaUkwasi(*LiquidityContingencyPlanning*) 51
6.6.1 Utangulizi 51
6.6.2 Viashiriavyamapemavyatahadhari 51
6.6.3 MkakatinaTaratibu(*StrategyandProcedures*) 52

CamScanner

6.7 Mapitiohuru(*IndependentReview*)....53
SEHEMU YA SABA
UDHIBITIWAKIHATARISHICHASOKO....54
7.1 Utangulizi....54
7.1.1 Kihatarishichakiwangochariba....54
7.1.2 Kihatarishichabei....54
7.1.3 Kihatarishichakubadilishafedhazakigeni....54
7.2 WajibuwaBodinaMenejimentiyaChama....54
7.2.1 WajibuwaBodi....55
7.2.2 WajibuwaMenejimentiyachama....55
7.3 SeranaTaratibu....56
7.4 VipimovyaVihatarishivyaSoko....57
7.5 UfuatiliajinaUkomo(*MonitoringandLimits*)....57
7.6 UanzishwajiwaBidhaanaHuduma mpya....57
7.7 MfumowaUsimamiziwaTEHAMA....58
7.8 Udhibitiwandani....58
7.9 MapitioHuru....58
7.10 UkaguziwaNdani....59
SEHEMUYANANE....59
USIMAMIZIWAVIHATARISHIVYAMATAKWAYAKISHERIA....59
8.1 Utangulizi....59
8.2 Bodi na Menejimenti....59
8.2.1 WajibuwaBodi....59
8.2.2 WajibuwaMenejimenti....60
8.3 SeranaTaratibu....61
8.4 UkaguziwaNdani....61
SEHEMUYATISA....63
USIMAMIZIWAVIHATARISHIVYAUWEKEZAJI....63
9.1 Utangulizi....63
9.2 WajibuwaBodiyaChamakatikaKudhibiti VihatarishivyaUwekezaji....63
9.3 MajukumuyaMenejimenti....63
9.4 MamboyaKuzingatiailiKudhibiti VihatarishivyaUwekezaji....64
SEHEMUYAKUMI....65
HITIMISHO....65

CamScanner

DIBAJI

Biashara ya fedha nchini imekuwa ikifanyika katika Nyanja/sekta mbalimbali ikiwemo Ija saccos ltd. Biashara hii inaweza kukumbwa na vihatarishi vingi ambavyo vinawezakusababisha kutofikiwa kwa malengo ya kimkakati ya chama na hivyo kusababisha hasara chamani. Kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa vihatarishi katikaChama kunaweza kuathiri uwekezaji wa Chama hivyo na kusababisha upotevu wa fedha za wanachama.

Mwongozo huu umeandaliwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 kifungu cha 12. Mwongozo huu umebainisha aina ya vihatarishi vinavyoweza kukumba na jinsi ya kuvitatua. Aidha, umeainisha maeneo makuu ya vihatarishi ambayo ni; matakwa ya kisheria, Soko na uwekezaji. Mwongozo huu utasaidia kubaini, kupima, na kuchukua hatua stahiki, pamoja na kufanya ufuatiliaji wa vihatarishi husika.

TANZANIA
Registered this 31st
day of January
Asst. Registrar

SURAYA KWANZA

UTANGULIZIWAMWONGOZOWAUSIMAMIZIWAVIHATARISHI

1.1 Utangulizi

Ija workers saccos ltd , kama ilivyo kwa taasisi nyingine zinazofanya biashara ya fedha nchini, inakumbana na vihatarishi vingi katika uendeshaji wa shughuli zake. Vihatarishi hivyo vinaweza kusababisha hasara kwenye uwekezaji unaofanywa na Chama na mwishoni chama hupata hasara ya biashara inayofanyika kwa mwaka husika. Hasara hizo zinaweza aidha kutarajiwa (kwa mfano hasara ya mikopo isiyolipika) au kutotarajiwa, kutegemeana na hali ya soko la fedha au mazingira yanayozunguka Chama (kwa mfano kushuka kwa uchumi, mabadiliko yaviwangovya riba, majanga au makosa ya kibinadamu).

Kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa vihatarishi kwenye Chama kunaweza: kuathiri uwekezaji wa Chama na kusababisha upotevu wa fedha zinazowekezwa na wanachama, na hivyo kutofikiwa kwa malengo ya kimkakati ya chama . Kutokana na hali hiyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na mfumo thabiti wa usimamizi wa vihatarishi kwenye Chama ambao utasaidia kubaini, kupima na kuchukua hatua stahiki pamoja na ufuatiliaji wa vihatarishi husika.

Hivyo basi, Ijaworkers saccos ltd imeandaa Mwongozo huu wa Usimamizi wa Vihatarishi kwa Chama ikiwa na lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa vihatarishi katika Chama

Mwongozo huu umezingatia viwango vya udhibiti wa vihatarishi vya kimataifa(International organization for Standardization- ISO 31000:2018) na umeainisha muundo na viwango vya msingi katika udhibiti wa vihatarishi. Hata hivyo, Mwongozo huu hauondoi matakwa ya Sheria zilizotungwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kanuni na Miongozo Mingine mbalimbali iliyotolewa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika kusimamia Vyama vya Ushirika wa Kifedha; badala yake unaongeza msisitizo wautekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo hiyo.

1.2 Lengo la Mwongozo

Mwongozo huu umeandaliwa na IJAWOSA LTD kwa lengo la kukielekeza Chama juu ya namna bora ya kudhibiti Vihatarishi kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vinavyokubalika ili kupunguza hasara na upotevu wafedha za wanachama na chama kutokufikia malengo yake.

Kwa mujibu wa Mwongozo huu, 'kihatarishi' ina maana ya uwezekano wa matokeo ya matendo au matukio yanayoweza kuleta athari katika mtaji, faida au fursa za chama husika. Matokeo hayo yanaweza kusababisha hasara moja kwa moja katika mapato au kushuka kwa mtaji na kusabisha chama kushindwa kufikia malengo yake. Kwa maana hiyo, Bodi na Watendaji wa Chama wanapaswa kuhakikisha kwamba panakuwepo na udhibiti imara wa

CamScanner

vihatarishi kulingana na hali halisi ya mazingira ya biashara ya chama . Vilevile, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani pamoja na kamati ya usimamizi vinategemewa kuhakikisha kwamba mazingira ya uendeshaji wa biashara ya chama yanazingatia uwepo wa mfumo thabiti wa usimamizi wa vihatarishi. Aidha, Wakaguzi wa nje wanapaswa kuhakikisha kwamba Mwongozo huu unazingatiwa katika uendeshaji na usimamizi wa vihatarishi kwenye Chama .

Usimamizi thabiti wa vihatarishi kwenye Chama unapaswa kuchukuliwa kama nyenzo muhimu katika utekelezaji wa mikakati na shughuli za Chama. Usimamizi bora na imara wa vihatarishi katika chama unapaswa kuzingatia utambuzi wa vihatarishi, upimaji wa vihatarishi, udhibiti na ufuatiliaji wa vihatarishi hivyo ili kuhakikisha kwamba:

i. Mhusikaanayesimamiaanaelewavizurivihatarishihivyo;

ii. Kiwango cha uhimilivu wa kihatarishi (*risk tolerance*) kipo ndani ya kikomo kilichowekwa na Bodi ya chama;

iii. Maamuzi yanayochukuliwa juu ya kihatarishi yanaendana na mikakati na malengo ya chama yaliyowekwa na Bodi;

iv. Maamuzi yanayochukuliwa juu ya kihatarishi yaende sawia na manufaa yanayotegemewa katika matokeo ya kihatarishi hicho;

v. Maamuzi juuyakihatarishiyawewazinayakueleweka;na

vi. Kuwepo kwa rasilimali/mtaji kwa ajili ya tahadhari ya vihatarishi vinavyoweza kujitokeza.

Mwongozo huu unatambua kuwepo kwa mazingira tofauti ya kibiashara, shughuli za chama, malengo na uwezo wa mtu mmoja mmoja katika Chama. Kutokana na tofauti hiyo, hakuna mfumo wa usimamizi wa vihatarishi unaoweza kudhibiti vihatarishi ; bali chama kinapaswa kuwa na mfumo mahususi wa Usimamizi wa Vihatarishi unaoendana na mazingira, shughuli, malengo na uwezo wa watumishi wake ambao utakuwa unahuishwa mara kwa mara.

1.3 UfafanuziwaVihatarishikatika Chama

Mwongozo huu umejumuisha maeneo kuu sita ya vihatarishi katika Chama ambayo ni; mikopo, ukwasi, soko, uendeshaji, mkakati na uzingatiwaji wa Sheria.

a) **Mikopo**: Ni uwezekano wa mkopaji kutokuwa na nia au uwezo wa kulipariba/mkopo au vyote viwili kwa mujibu wa mkataba au makubaliano ya ukopeshajiwa mkopo huo, na hivyo kusababisha hasara kwa chama.

b) **Ukwasi**: Ni pale chama kinaposhindwa kutimiza au kulipa madeni/dhima za muda mfupikwa wakatizinapotakiwa kulipwa.Hiiinajumuisha chama kutokuwa na uwezo wa kukabiliana na upungufu usiotarajiwa au mabadiliko ya vyanzo vya fedha. Vilevile, kihatarishi hiki kinatokana na chama kushindwa kutambua mabadiliko ya soko ambayo yanaathiri mali zisizo za kifedha kubadilishwa kwa haraka kuwa fedha.

CamScanner

c) **Soko:** Hii hutokea kutokana na mabadiliko ya bei za soko, viwango vya riba pamoja na ubadilishaji wa fedha za kigeni.

d) **Uendeshaji:** Hii hutokana na upungufu katika muundo wa kiuendeshaji, udhibiti wa ndani, watendaji wa vyama, mfumo wa usimamizi wa taarifa au matukio ya nje yanayojumuisha vihatarishi vya Kisheria.

e) **Mkakati:** Hii hutokana na athari za sasa na zinazotarajiwa kutokea kwenye Mapato, mtaji na taswira (reputation/image) ya chama kutokana na maamuzi mabaya ya kibiashara yanayofanywa na uongozi, utekelezaji wa maamuzi yasiyofaa, uwepo wa mabadiliko ya kiuchumi au teknolojia.

f) **Uzingatiwaji wa Sheria:** Kinatokana na athari za sasa na zinazotarajiwa kwenye mapato, mtaji, taswira ya chama na ukiukwaji au kutokuzangatiwa kwa Sheria, Kanuni, Mikataba, kutokana na tafsri zisizo sahihi za Sheria au Kanuni husika.

1.4 MpangowaUsimamiziwa Vihatarishi

Chama kinaweza kuwa na mfumo tofauti wa usimamizi wa vihatarishi kulingana na ukubwa wa chama na aina ya shughuli za kibiashara ambazo chama kinafanya. Hivyo, chama kinatakiwa kuandaa mpango mahsusi wa usimamizi wa vihatarishi utakaokidhi mahitaji na mazingira ya utendaji wa chama . Mpango huo unategemewa ufanyiwe mapitio angalau mara moja kwa mwaka. Vilevile, mipango yote inapaswa kuzingatiaangalau vihatarishi sita vilivyoanishwa katika mpango huu.

1.5 Usimamizi wa Vihatarishi

Usimamizi wa Vihatarishi ni utaratibu wa kubaini, kupima, kudhibiti pamoja na kufuatilia vihatarishi katika Chama. Hii inaweza ikafanikiwa kwa kuweka juhudi za makusudi katika kuanzisha muundo madhubuti wa Mwongozo wa Usimamizi wa Vihatarishi ambao utawezesha mazingira rafiki ya kubaini vihatarishi katika miamala na mfumo wa chama kwa ujumla. Usimamizi wa Vihatarishi unazingitia hatua zifuatazo;

a) **Uhimilivu wa kihatarishi (*risk tolerance*):** Hiki ni kiwango ambacho Bodi na Menejimenti wako tayari kukivumilia katika kufikia malengo ya kibiashara. Mara nyingi kiwango hiki kiko katika sera mbalimbali za chama pamoja na Kanuni na mipango ya chama. Sera hizo hutoa maelezo ya mawanda kwa watendaji katika kufanya maamuzi juu ya miamala mbalimbali na shughuli za chama kwa ujumla ambazo ziko ndani ya wigo wa kiwango cha kihatarishi husika.

b) **Utambuzi wa kihatarishi (*risk identification*):** Ni hatua ambayo miamala, matukio nashughulizachamazenyevihatarishihubainishwanakutambuliwana Menejimenti ya chama. Ili chama kiweze kutatua kihatarishi ni lazima kiwe na mifumo imara na mbinu za kubaini vihatarishi kwa kila hatua ya miamala nashughuli za chama kwa ujumla. Zoezi hili ni lazima liwe endelevu kwa kuhakikisha kuwa vihatarishi vilivyopo na vinavyotazamiwa vinabainishwa mara moja.

CamScanner

c) **Upimaji wa Vihatarishi (*risk measurement*):** Hii ni hatua ya tathmini ya athari za vihatarishi katika ngazi ya miamala, matukio au katika shughuliza chama. Uwiano wa vihatarishi ni nyenzo muhimu inayotumika kupima na kuonesha mwelekeo wa kihatarishi husika. Mfumo wa usimamizi wa taarifa za chama unapaswa kutoa taarifa kwa uongozi wa chama kuhusu kiwango na athari za vihatarishi zinazokabilishughuli za chama. Kila chama kinapaswa kuangalia mwenendo wa vihatarishi kulingana na shughuli na mazingira yake. Viashiria hivyo vinapaswa kufanyiwa mapitio kwa muda maalumu ili kubaini athari zake.

d) **Udhibiti wa Vihatarishi (*risks control*):** Ni viwango vya udhibiti vinavyowekwa na menejimenti ya chama kwenye sera, mfumo wa udhibiti wa ndani, ukaguzi wa ndani, muundo wa uongozi na wafanyakazi kwa ujumla; ili kuhakikisha kuwa vihatarishivya chama vipo katika wigo himilivu wa kiwango kinachokubalika cha kihatarishi husika. Chama kitapaswa kuwa na mfumo wa mabadiliko ambao utategemea utambuzi na matokeo ya vihatarishi katika chama.

e) **Ufuatiliaji wa Vihatarishi (*risk monitoring*):** Hii ni hatua endelevu inayotumika katika kubaini mabadiliko ya viwango vya vihatarishi na kuhakikisha usimamizi na udhibiti wa vihatarishi unazingatiwa. Kila chama kinapaswa kuwa na mfumo imarana madhubuti wa usimaizi wa taarifa pamoja na Mkaguzi wa Ndani katika kuhakikisha kuwa kuna ufuatiliaji wa viashiria na matokeo ya vihatarishi. Vilevile, chama kinapaswa kutoa taarifa sahihi kwa wakati kwa wahusika ili wawezekuchukua hatua za haraka pale inapohitajika ili kukabiliana na vihatarishi husika.

1.6 MamboMuhimu yaKuzingatiakatikaUandaajiwaMuundowaUsimamiziwa Vihatarishi

Ili chama kiwe na mfumo madhubuti na thabiti wa usimamizi wa vihatarishi, kinapaswa kuzingatia mawanda mapana ya vihatarishi, hatua na mchakato wa kudhibiti vihatarishi, majukumu na wajibu wa kila mhusika katika kusimamia na kudhibiti vihatarishi. Mfumo huo unapaswa kuwa jumuishi kwa kiwango cha kutosha ili kuhakikisha kuwa kila aina ya vihatarishi vinavyokikabili chama vinabainishwa na kudhibitiwa ipasavyo. Vile vile, mfumo huounapaswakuruhusumabadiliko ilikukabiliananamabadilikoyamazingirayakibiashara. Muundo wa usimamizi unapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

(a) BodinaMenejimentiimarakatikausimamizina uangaliziwa chama;

(b) Kitengochausimamizi/msimamiziwavihatarishikatika chama;

(c) Sera,kanuni, taratibuna ukomo (limits);

(d) Upimajitoshelevuwavihatarishi, ufuatiliajinamfumo wausimamiziwa taarifa;

(e) Mfumo wandaniwaudhibitiunaojitosheleza;

(f) Mapitiohuru yamfumowausimamiziwa vihatarishi;

(g) Mfumojumuishi wausimamiziwaVihatarishi; na

CamScanner

(h) Mpangowadharulajuuyavihatarishi.

1.6.1 BodinaMenejimentikatikausimamiziwachama

1.6.1.1 Majukumuya Bodiyachama

Bodiyachamainajukumulausimamiziwavihatarishivinavyokikabilichamakama ifuatavyo:

a) Kupitisha shughuli zote za mikakati ya kibiashara na sera muhimu za chama husikaikijumuisha mambo yote yanayohusiana na usimamizi wa vihatarishi;

b) Kuhakikisha kwamba watendaji wakuu wa chama wanatekeleza hatua zote za udhibiti na usimamizi na sera zinazohusika katika usimamizi wa vihatarishi; na

c) Kuhakikishakwambawatendajiwakuuwanauwezowakutoshakatikakusimamia shughuli za kibiashara zinazoendeshwa na chama.

Kwa maana hiyo, Wajumbe wote wa Bodi ya chama wanapaswa kuwajibika na kuelewa asili ya vihatarishi vyote vikubwa vilivyopo kwenye chama na kuhakikisha kwamba menejimenti inachukua hatua muhimu za kutambua, kupima, kufuatilia na kudhibiti vihatarishi hivyo.Kwa muktadha huo, Bodi ya chama inapaswa kupokea taarifa mara kwa mara kutoka kwa menejimentiinayoainishaasili,kiwangonaukubwawavihatarishivinavyokabilichamachao, na kwa wakati huo, Bodi inapaswa kutoa sera na miongozo inayokubalika katika kusimamia vihatarishi hivyo.

1.6.1.2 WajibuwaMenejimentiya Chama

a) Kutekeleza mikakati katika namna ya kuhakikisha ukomo unaohusiana na usimamizi wa vihatarishi unazingatiwa. Menejimenti inapaswa kuwa na maarifa na ujuzi wa kutosha kuhusiana na shughuli muhimu za biashara zao, ili kuhakikisha kwamba sera stahiki, viwango vya udhibiti, na mifumo ya ufuatiliaji wa vihatarishi vinakuwepo na kwamba mgawanyo wa majukumu kwa kila mmoja unajulikana ipasavyo.

b) Kuanzisha mawasiliano na uelewa mpana wa mahitaji muhimu wa mfumo madhubuti wa ndani na viwango vya juu vya maadili. Ili kutimiza wajibu huo, menejimenti ya chama inapaswa kuhakikisha kuwa inaelewa kwa ufasaha mabadiliko na maendeleo katika sekta ya kifedha na shughuli zinazoendeshwa na chama, ikiwa ni pamoja na kuelewa mfumo wa udhibiti wa ndani mahususi katika usimamizi wa vihatarishi.

1.6.1.3 Kitengochausimamizi/msimamizi wavihatarishikatikachama

Ili chama kiwe na udhibiti wa vihatarishi, kinapaswa kuwa na kitengo mahsusi (kutegemeana na ukubwa wa shughuli zinazoendeshwa) au afisa wa chama atakayehusika katika kusimamia vihatarishi kwenye chama. Majukumu ya kitengo hicho au Afisa huyo yatakuwa ni:

a) Kutambuavihatarishivilivyoponavitakavyoweza kujitokeza;

CS CamScanner

b) Kutengenezamfumowauchambuzinaupimajiwavihatarishi;

c) Kuanzishasera, taratibunambinuzaudhibiti wausimamizi wavihatarishi;

d) Kutengeneza viwango himilivu vya vihatarishi kwa vitakavyopitishwa naMenejimenti na Bodi;

e) Kufanya Ufuatiliaji wa viwango himilivu vya vihatarishi vilivyoidhinishwa na kukubalika; na

f) Kutoa taarifa ya matokeo juu ya ufuatiliaji wa vihatarishi kwa Menejimenti na Bodiya Chama.

1.6.2 Sera,kanuni,taratibunaukomo/mipaka

Bodi ya chama na menejimenti wanapaswa kuandaa sera, kanuni na taratibu kuendana na mwongozo wa usimamizi wa vihatarishi vinavyokikabili chama. Iwapo vihatarishi vitabainishwa, sera, kanuni na taratibu za chama zitatoa mwongozo wa kukabiliana na vihatarishi hivyo kulingana na shughuli za kila siku za chama. Sera, Kanuni na taratibu za chama hazina budi:

a) Kuwa na uwezo wa kutambua kwa wakati, kupima, kufuatilia, kudhibiti vihatarishi katika uwekezaji, biashara na shughuli nyingine muhimu za chama kwa ngazi ya miamala na chama kwa ujumla;

b) Kuhakikisha kuwa vihatarishi vya kiuchumi vinatambuliwa kikamilifu na kujumuishwa katika mfumo wa chama wa usimamizi wa vihatarishi;

c) Kuzingatiamalengo makuuyachamapamojanauwezo wakifedhawa chama;

d) Kuzingatia mgawanyo wa majukumu katika uwajibikaji na utekelezaji wa shughuli za chama na kuhakikisha uwepo wa uwazi wa mgawanyo wa majukumu katika kusimamia vihatarishi;

e) Kutambua na kushughulikia kwa haraka maeneo ya vihatarishi yaliyozidi viwangovya ukomo wa vihatarishi;

f) Kufanya mapitio ya biashara na bidhaa mpya kwa kuweka pamoja mifumo ya usimamizi wa vihatarishi na bidhaa ili kuhakikisha kuwa chama kinasimamia na kudhibiti shughuli hizo kabla ya kuanzishwa; na

g) Kujumuisha maelezo na hatua za mapitio ya sera, kanuni na mipaka ya maamuzi katika vihatarishi na kuzihuisha ipasavyo.

1.6.3 Upimajitoshelevuwa vihatarishi,ufuatiliaji namfumowausimamiziwa taarifa

Chama kinapaswa kuwa na mfumo thabiti wa ufuatiliaji wa vihatarishi vilivyotambuliwa na kupimwa athari zake. Mfumo huo unatakiwa kusaidiwa na mfumo wa usimamizi wa taarifaza chama ili kuweza kutoa taarifa sahihi na kwa wakati kwa Bodi ya chama na Menejimenti kuhusianananahaliyafedha,matokeoyauendeshajinataarifazavihatarishivinavyokikabili

CamScanner

chama, ikiwa ni pamoja na utoaji wa taarifa mara kwa mara kuhusiana na utekelezaji wa shughuli za kila siku za chama kwa kila ngazi za utawala.

Ili kuhakikisha uwepo wa mfumo thabiti wa upimaji, ufuatiliaji na usimamizi wa taarifa za chama, mambo yafuatayo ni muhimu kuzingatiwa:

a) Mfumo wa chama wa ufuatiliaji wa vihatarishi na taarifa unapaswa kubainisha vihatarishi vyote vinavyokikabili chama;

b) Vyanzo vya taarifa, mchakato wa upimaji na ufuatiliaji wa vihatarishi unapaswa kuandikwa kwa ufasaha na usahihi ili kutoa mwanya wa kupima ufanisi wake mara kwa mara;

c) Kuhakikisha kuwa taarifa na mifumo mingine ya mawasiliano inashabihiana na shughuli za chama zenye mlengo wa ufuatiliaji wa vihatarishi na uzingatiaji wa mipaka/ukomo, malengo au madhumuni ipasavyo, kwa kulinganisha matokeo halisina tarajiwa; na

d) Utoaji wa taarifa kamili na kwa wakati kwa Bodi na menejimenti ya chama wenye kuwezesha kufanya maamuzi sahihibaada ya kutambua mwenendo hasi ndani ya Chama

1.6.4 Mfumothabiti waudhibiti wa ndani

Mfumo thabiti wa udhibiti wa ndani ni nyenzo muhimu katika udhibiti wa vihatarishi na usimamizi wa mali za chama. Kuanzisha na kusimamia mfumo wa udhibiti wa ndani unaojumuisha mgawanyo wa majukumu na mipaka ya utendaji ni jukumu muhimu la menejimenti ya chama. Mfumo wa udhibiti wa ndani ukiwa imara na fanisi utasaidia utunzaji sahihi wa mali za chama, uzingatiwaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali, pamoja na utoaji wa taarifa sahihi za fedha. Mfumo huu hauna budi kufanyiwa mapitio na mkaguzi wa ndani ambaye atatoa taarifa moja kwa moja kwenye Bodi ya chama husika. Vile vile, upungufu utakaobainishwa na mkaguzi wa ndani yanapaswa kuandikwa kikamilifu na kuwasilishwa kwenye menejimenti kwa ajili ya uboreshaji au marekebisho ya upungufu huo ili kuleta ufanisi katika mifumo ya udhibiti.

Ili kuhakikisha kuwa panakuwepo na ufanisi katika mfumo wa udhibiti wa ndani na hatua za ukaguzi, chama kinapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

a) Mfumo wa udhibiti wa ndani unapaswa kuendana na aina na kiwango cha vihatarishi vinavyokikabili chama kwa kuzingatia shughuli zake;

b) Muundo wa chama unapaswa kuweka mipaka ya kiutendaji na uwajibikaji kwa ajiliya ufuatiliaji, inayozingatia sera, kanuni na ukomo wa vihatarishi;

c) Mfumo wa utoaji wa taarifa za chama unapaswa kuwa huru katika ngazi zote za udhibiti kulingana na mgawanyo wa majukumu na mipaka ya kiutendaji;

CamScanner

d) Mfumo wa utoaji wa taarifa za fedha, matokeo ya utendaji na taarifa za usimamizi wa chama unapaswa kuaminika, kuwa sahihi na kutoa taarifa kwa wakati, na tofauti yoyote itakayobainika haina budi kufuatiliwa na kufanyiwa kazi mara moja;

e) KuwepokwataratibuzauzingatiajiwaSherianaKanuni;

f) Mkaguzi wa ndani anapaswa kutoa maoni huru katika mfumo wa udhibiti wa ndani;na

g) Kamati ya usimamizi inapaswa kufanya mapitio ya ufanisi wa mifumo ya ukaguzi wa ndani na shughuli mbalimbali za udhibiti mara kwa mara.

1.6.5 Mapitiohuruyamfumo wausimamiziwa vihatarishi

Mwongozo wa usimamizi wa vihatarishi unapaswa kufanyiwa mapitio huru ya ufanisi ili kubaini uzingatiaji wa sera na taratibu za mwongozo huo wa chama. Mapitio hayo yanaweza kufanywa na Mkaguzi wa ndani, Mkaguzi wa nje au mtu yeyote au mamlaka ambayo inapaswa kuwa huru katika utekelezaji wa mwongozo huo na anapaswa kutoa taarifa moja kwa moja kwa Bodi au kamati iliyoteuliwa. Ili kuwepo ufanisi wa mapitio, mpitiaji anapaswa kuwa na nguvu kimamlaka, ujuzi na utaalamu kwamba matokeo na mapendekezo ya mapitio yake yatatekelezwa pasipo pingamizi. Mpitiaji huru, pamoja na mambo mengine, anapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

a) Mwongozo wa usimamizi wa vihatarishi unaendana na chama pamoja na shughuli zake;

b) Chamakinakitengo/afisa huruanayeshughulikanavihatarishivya chama;

c) Bodina menejimentiya chama inahusikakatikahatua zausimamizi wavihatarishi;

d) Sera, udhibiti na kanuni zinazohusu usimamizi wa udhibiti wa vihatarishi zimeandikwa, zinajulikana na kuzingatiwa; na

e) Chama kina watumishi wanaoelewa mfumo thabiti wa usimamizi wa udhibiti wa vihatarishi.

1.6.6 Mfumo jumuishi wausimamizi wa vihatarishi

Vihatarishi havitakiwi kuangaliwa katika mtazamo/mlengo mmoja kwa kuwa kihatarishi kimoja kinaweza kusabishwa na au kusabisha kihatarishi kingine. Kwa hiyo, mwongozo wa usimamizi wa vihatarishi unatakiwa kutambua na kuakisi muingiliano wa vihatarishi wa shughuli zote za chama kwa ukamilifu. Wakati wa kutathmini na kusimamia vihatarishi, menejimenti inapaswa kuwa na uwezo wa kuangalia kwa upana vihatarishi vinavyokikabili chama. Hivyo, chama kinapaswa kuwa na mfumo utakaoangalia mahusiano ya vihatarishi vilivyopo kwenye shughuli za chama kwa ujumla.

1.6.7 Mpangowadharurajuu ya vihatarishi

Chama kinapaswa kuwa na utaratibu wa kubaini changamoto zilizopo mbeleni na kupanga jinsiyakuzikabilikatikamudamuafakanakwaufanisi.Kwamfano,shughulizampangowa

dharura zitajumuisha; mpango wa udhibiti wa majanga, mkakati wa kukabiliana na kesi, mkakati wa kukabiliana na ukwasi na mikakati inayojibu mabadiliko ya kisheria. Mpango wa dharura unapaswa kufanyiwa mapitio ya mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa unajumuisha matukio yanayoweza kujitokeza na kuathiri shughuli za chama.

SEHEMUYAPILI

USIMAMIZIWAKIHATARISHICHA MIKOPO

2.1 Utangulizi

Mikopo ndiyo kitovu cha shughuli za Chama. Hivyo, chama hakina budi kuweka sera madhubuti za usimamizi wa eneo hili ili kuhakikisha kuwa mikopo inayotolewa na chama inarejeshwa ipasavyo. Kwa kuzingatia hilo, IJAWOSA LTD imeona umuhimu wa kuandaa 'Mwongozo wa Usimamizi wa Vihatarishi' ili kuviwezesha Chama kuepukana na vihatarishi hivyo na hivyo kuviwezesha kufikia malengo yake.

Vihatarishi vya mikopo ni uwezekano wa wakopaji kutokuwa na nia au uwezo wa kulipariba, mkopo au vyote viwili kwa mujibu wa mikataba au makubaliano ya ukopeshaji wa mkopo huo na kusababisha hasara kwa chama. Chanzo cha kihatarishi hiki ni kutokufuata taratibu katika mchakato wa utoaji na ufuatiliaji wa mikopo ikiwa ni pamoja na mrundikano wa mikopo kwa mtu mmoja, kikundi au taasisi zinazohusiana au kutokana

Vihatarishi vya mkopo vinaweza kusabishwa na au kusababisha kihatarishi kingine katika chama, na hivyo kuathiri shughuli za chama kwa ujumla; kwa mfano kihatarishi kutokana na mikopomibayakinawezakusababishavihatarishi vyaukwasi.Hivyo,chamakinapaswakuwa makini na kuchukua hatua madhubuti katika kudhibiti vihatarishi.

Sehemu hii inaonesha misingi ya sera ya usimamizi wa vihatarishi vya mikopo ambayo kila chama kinapaswa kuwa nayo. Mwongozo umeainisha misingi inayokubalika ambayo imeeleza kwa kina, utaratibu wa ukopeshaji unaotakiwa kuandaliwa na kutekelezwa navyama husika.

2.2 WajibuwaBodinaMenejimentikatikaKusimamia Vihatarishi

2.2.1 Wajibu wa bodi

Bodi ya chama ina wajibu wa kuidhinisha na kufanya mapitio ya mikakati na sera za vihatarishi vya mikopo ya chama. Ni jukumu la Bodi kuhakikisha kuwa Mkakati wa kihatarishichamikopounawekawazikwambauhimilivuwakihatarishiunapaswakukubalika chamani kwa lengo la kufikia kiwango cha faida kinachotarajiwa kutokana na kihatarishi cha mikopo. Sera ya mikopo inapaswa kuwa toshelevu na inayojumuisha shughuli zote ambazo zina vihatarishi vya mikopo.

Majukumu mahususi ya Bodi ya chama katika usimamizi wa vihatarishi vya mikopo ni pamoja na;

a) Kufafanuakwaujumlauhimilivuwaviwangovyavihatarishivinavyohusianana mikopo,

b) Kuhakikishakwamba mipango thabiti,sera na taratibuza usimamiziwavihatarishi vya mikopo zinaandaliwa na kutekelezwa,

CamScanner

c) Kuhakikisha kwamba menejimenti na watendaji wengine wanaohusika na utoaji wa mikopo na usimamizi wa vihatarishi wanakuwa na ujuzi na weledi wa kutekeleza majukumu yao,

d) Kuhakikisha kwamba vihatarishi muhimu vya mikopo vinazingatiwa katika viwango vinavyokubalika kuendana na mtaji wa chama,

e) Kufanya mapitio ya vihatarishi kwa watu wa ndani pamoja na watu wenye uhusiano/ukaribu, ikijumuisha sera zinazohusiana nao,

f) Kufahamu na kuvifanyia kazi vihatarishi vinavyozidi kiwango kinachotakiwa kusimamiwa na menejimenti,

g) Kufanya mapitio ya mwenendo wa ubora wa mikopo na utoshelevu wa matengo ya hasara ya mikopo.

h) Kubainishamarakwamarataarifazausimamiziwavihatarishizinazotakiwakutolewa na menejimenti kwenye Bodi, na

i) Kuhakikisha kwamba mkaguzi wa ndani anafanya mapitio ya shughuli za mikopo ili kutathmini iwapo sera na taratibu za chama ni sahihi na zinatekelezwa.

2.2.2 Kamati yamikopo

Kwa mujibu wa Kanuni ya 26 ya Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha, chama kitapaswa kuchagua kamati ya mikopo ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia shughuli za utoaji wa mikopo katika chama. Majukumu ya kamati ya mikopo katika usimamizi wa vihatarishi vya mikopo ni pamoja:

a) Utekelezajiwaserayavihatarishi vyamkopoiliyoidhinishwanaBodi;

b) Ufuatiliaji wa vihatarishi vya mikopo ili kuhakikisha kuwa vihatarishi hivyovinakuwa ndani ya ukomo uliowekwa na Bodi;

c) KupendekezaserayaviwangovyamikoponakuiwasilishakwenyeBodi kwahatua za uidhinishwaji; na

d) Kupendekeza kiwango cha juu cha uidhinishaji wa mikopo utakaofanya kwa niaba ya kamati, ukomo wa mikopo mikubwa, viwango vya dhamana za mikopo, utaratibu wa ukaguzi wa mikopo, viwango vya vihatarishi katika mikopo, ufuatiliaji na tathmini, gharama za mikopo na uzingatiaji wa sheria na taratibu.

2.2.3 Menejimenti

Usimamizi wa vihatarishi vya mikopo utafanywa na Menejimenti kwa niaba ya Bodi ya Chama. Majukumu ya Menejimenti ni kuhakikisha kuwa sera, miongozo na taratibu zilizowekwa na Bodi zinafuatwa katika usimamizi wa vihatarishi vya mikopo. Majukumu mahususi ya menejimenti katika usimamizi wa vihatarishi vya mkopo ni pamoja na:

a) Kuandaa sera ya mikopo na taratibu za usimimizi wa mikopo na kuiwasilisha kwenye Bodi ya chama kwa ajili ya kuidhinishwa;

CamScanner

b) Kusimamiautekelezaji waserayausimamizi wavihatarishi katika mikopo;

c) Kutengenezanakutumiamfumo sahihi wautoaji wataarifa;

d) Kufuatilia na kudhibiti aina na muundo wa mikopo inayotolewa na chama kwa kuzingatia matakwa ya Sheria na Kanuni;

e) Kufuatilia ubora wa mikopo na kuhakikisha kuwa matengo ya mikopo mibaya yanawekwa;

f) Kuhakikisha kuwa utafiti wa bidhaa mpya unafanyika kwa usahihi ili kuvitambua na kuvidhibiti vihatarishi vinavyoweza kujitokeza;

g) Kuanzisha mfumo wa udhibiti wa ndani na kuweka utaratibu mzuri wa mamlaka na uwajibikaji;

h) Kusimamia usambazaji wa sera na taratibu za usimamizi wa vihatarishi na taarifa ya usimamizi wa vihatarishi vya mkopo kwa watumishi wanaoshughulikia masuala ya mikopo; na

i) Kuhakikisha ukaguzi wa ndani wa mfumo wa usimamizi wa vihatarishi vya mikopo unafanywa mara kwa mara.

2.3 Mkakatiwa UanzishajinaUendelezajiwa Bidhaa

Chama kinachotaka kuanzisha bidhaa mpya kinatakiwa kufanya tathmini ya bidhaa hiyokama itaisaidia kufikia malengo ya kifedha, kiushindani, kijamii na malengo ya chama kwa ujumla.

Endapo chama kitaona kuwa bidhaa inayokusudiwa kuanzishwa inaendana na malengo hayo, kitapaswa kufanya tathmini ya uwezo wake katika kushughulikia bidhaa mpya. Mambo ya kuzingatia wakati wa kufanya tathmini hiyo ni pamoja na uwezo wa watumishi, njia za utoaji huduma, mifumo ya usimamizi na mafunzo. Aidha, chama kitatakiwa kufanya tathmini juuya athari za bidhaa mpya kwenye eneo la utoaji wa mikopo na ukwasi wa chama.

Taratibuzakuzingatia wakati wakuanzisha bidhaampyani:

i. Tathminikatikachama

- Kufanya tathmini ya uwezo wa chama na utayari katika kuanzisha bidhaa mpya, na
- Kufanya tathminiya bidhaa mpya kwa kuzingatiabei,taratibu,udhibiti wa ndani, soko na usimamizi wa vihatarishi.

ii. Utafiti wa Masoko

- Kukusanya na kutathmini takwimu za masoko sinazohusiana na bidhaa mpya, kwa mfano, mahitaji ya bidhaa na hali halisi ya bidhaa zinazofanana na bidhaa mpya zinazotolewa na washindani, na

CamScanner

- Kufanya utafiti wa awali wa soko kwa kuangalia hali ya wateja wa chama waliopo na wanaotarajiwa.

iii. ***SifazabidhaanaUpatikanaji wake***

- Kutoamaelezoyabidhaa,
- Kutengeneza mfumo wa utoaji wa huduma, taratibu na mfumo wa usimamizi wa taarifa,
- Kufanyatathmini ya makadirio yamapato na matumizi, na
- Kutoaufafanuzi juu yauzingatiwajiwaSherianaKanuni.

iv. ***Majaribio ya bidhaa***

- Kufaafanua malengo ya majaribio ya bidhaa na ufuatiliaji wakati wa majaribio kulingana na malengo ya utendaji na makadirio ya kifedha;
- Kuweeka vigezo vya majaribio ya bidhaa ikiwa ni pamoja na eneo, muda, na tarehe ya tathmini;
- Kufuatilianakutathmini matokeoyamajaribio ya bidhaa; na
- Kuandaa taarifa ya matokeo ya majaribio, ikilinganishwa na matarajio, kile walichojifunza, mifumo ya usimamizi na mpango wa utekelezaji.

v. ***Utoaji wa bidhaa***

- Kutoa taarifa kwa wanachama juu ya bidhaa mpya iliyofanyiwamajaribio;
- Kuingizabidhaampya sokoni;
- Kuandaabajeti ya utoajiwahuduma,ratibanamfumo waufuatiliaji;
- Kuweka mfumo wa utoaji wa bidhaa, kukamilisha mwongozo wa utoaji wa huduma, na kutoa mafunzo kwa watendaji wa chama juu ya bidhaa husika; na
- Kufuatilia na kutathmini mchakato wa utoaji wa bidhaa mpya na kufanya maboresho ya huduma kulingana na matokeo ya tathmini.

2.4 Sera,TaratibunaMipaka/Ukomo

2.4.1 SerayaMikopo

Sera ya mikopo ni nyenzo muhimu katika usimamizi wa vihatarishi vya mikopo na hutoa msingi mzuri wa usimamizi wa mikopo katika chama. Sera ya mikopo inapaswa kuweka vigezona miongozoyautoaji,ufuatiliajinausimamiziwamikopokatikangaziyamtubinafsi na mikopo yote ya chama kwa ujumla. Katika kushughulikia masuala yote muhimu ya mikopo, sera ya mikopo inapaswa kujumuisha mambo yafuatayo:

a) Aina za mikopo inayotolewa, riba, malengo ya faida, muda wa ukomo wa marejesho ya mikopo viwango vya juu vya kuhudumia deni kwa kila aina ya mkopo;

b) Kiwango cha juu cha jumla ya mikopo inayotolewa kwa kuzingatia uwiano wamikopo kwa amana au hisa za hiari kwa Vyama vyenye Leseni daraja A au asilimiaya mtaji;

c) Ukomo wa utoaji wa mikopo kwa kuzingatia sekta, aina ya mkopaji na aina yabidhaa;

d) Aina za dhamana zinazokubalika kwa kuzingatia uwiano wa thamani ya mkopo kwa thamani ya dhamana na vigezo vinavyokukubalika kwa udhamini.

e) Mipakayauidhinishajiwa mikopo;

f) Ukasimishwajiwamamlakayauidhinishajiwamkopo kwawatendaji wa chama;

g) Taratibuzauhakikiwa maombi yamikopo pamojanauidhinishaji wamikopo;

h) Uainishaji na usimamizi wa matatizo katika mikopo na kufanya matengo ya mikopo mibaya;

i) Utoaji wa taarifa zinazohusiana na mikopo kamavile utakatishaji wa fedha haramu na uzingatiwaji wa matakwa ya kisheria kwa waombaji wa mikopo;

j) Utaratibuwaukusanyajiwamikopo; na

k) Chama kinapaswa kuhakikisha kuwa sera na taratibu za kusimamia mikopo zinatayarishwa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika. Ili kuwa na ufanisi, sera ya mikopo inatakiwa kuwasilishwa kwa wahusika wote ndani ya chama ili kutekeleza taratibu zilizoainishwa kwenye sera. Aidha, sera ya mikopo itatakiwa kufanyiwa marekebisho mara kwa mara ili kuendana na mabadiliko ya ndani na nje ya chama.

2.4.2 Mgawanyowa majukumu

Uandaaji wa Sera ya Mikopo, uwekaji wa mipaka katika mikopo, ufuatiliaji wa mikopo na upitiaji wa nyaraka mbalimbali zinazohusiana na mikopo ni kazi ambazo zinapaswakufanywa na watu tofauti na waliopo kwenye kitengo cha mikopo cha chama husika. Kwa Vyama ambavyo ni vidogo na vinashindwa kufuata utaratibu huu, vitatakiwa kuweka utaratibu mzuri ili kudumisha nidhamu katika usimamizi wa mikopo na hivyo kuzuia migongano ya kimaslahi.

2.4.3 Bidhaa za mikopo

Chama kitapaswa kuwa na nyaraka ambazo zitaainisha aina ya bidhaa za mikopo zitakazotolewa na chama. Menejimenti ya chama ni lazima iwe na uelewa mzuri juu yabidhaa zinazotolewa na chama na kusimamia vihatarishi vilivyopo na vinavyoweza kutokea. Pia,chamakitapaswakuainisha ukomonamudawa mikopo.Menejimentiyachamaitapaswa

CamScanner

kufanya utafiti wa bidhaa mpya na kuiwasilisha kwenye Bodi ya chama kwa ajili ya kuidhinishwa kabla ya kuwasilishwa kwa wanachama.

2.4.4 Utaratibuwautoajiwamikopo

Chama kitatakiwa kuwa na sera ambazo zimeainisha vigezo na utaratibu wa utoaji wa mikopo. Vigezo hivyo vitapaswakujumuisha sifa zawakopaji, lengolamkopo na chanzo cha kulipa mkopo huo. Chama kinatakiwa kuwa na taarifa za kutosha kuhusiana na sifa za wakopaji ili kuwezesha kufanya tathmini ya vihatarishi vya wakopaji husika.

Serakatikaeneo lautoajiwamikopoinatakiwakuanisha mambo yafuatayo:

a) Madhumuni nachanzochaulipajimikopo;

b) Sifazamkopaji;

c) Hali ya vihatarishi vya mkopaji na athari zake kwenye sekta husika na Uchumi kwaujumla;

d) Historiayamkopaji kuhusu ulipaji nauwezowakewa kifedha;

e) Taarifa za mkopaji kutoka kwenye mfumo wa taarifa za wakopaji (*Credit ReferenceBureau)*;

f) Uwezowakuwajibika kisheriakwadhamana zilizowekwanamkopaji;

g) Kwa mikopo ya biashara, ni kuangalia utaalamu wa biashara wa mkopaji na sekta ya kiuchumi ya mkopaji;

h) Masharti na vigezo vya mkopo pamoja na masharti yanayoweza kubadilika kutokana na mabadiliko katika vihatarishi vya mkopo husika; na

i) Utoshelevunausimamiziwadhamanazawakopaji.

Mamlaka ya ukopeshaji yaliyokasimishwa kwa Menejimenti ya chama ni lazima yawe kwa maandishi. Ni muhimu kujumuisha taratibu za utoaji wa taarifa kwa kamati mbalimbali na maafisa wanaoshughulikia mikopo.

Aidha, usimamizi wautaoaji wamikopo unapaswakubainishwa ili kujiridhishakama taratibu hizo zimezingatiwa. Vilevile, mikopo inayotolewa kwa Wajumbe wa Bodi na watendaji wa chama haina budi kuzingatia taratibu za utoaji wa mikopo zilizowekwa na chama.

2.4.5 Ufuatiliajiwa wakopaji

Chama kinapaswa kuwa na mfumo wa ufuatiliaji wa hali ya mikopo iliyotolewa. Viashiriavya hali ya mikopo vinapaswa kuanishwa na kufuatiliwa ili kukiwezesha chama kubaini changamoto zinazojitokeza na kuzitolea taarifa. Viashiria hivyo vitakuwa katika maeneo yafuatayo:

a) **Haliya kifedhana kibiashara**

Chama kinapaswa kufanya tathmini ya hali ya kifedha, mtaji na uwezo wa kibiashara wa mkopaji.

b) **Mwenendowahesabuza mkopaji**

Chama kinapaswa kufuatilia marejesho ya mkopo na malipo ya riba na shughuliza mkopaji.

c) **MakubalianoyaMkopo**

Chama kinapaswa kufuatilia utekelezaji wa makubaliano yaliyopo kwenye mkataba wa mkopo.

d) **Uthaminishajiwadhamanazamikopo**

Chama kinapaswa kuthaminisha dhamana za mikopo mara kwa mara ili ziendane na mabadiliko ya soko. Kwa mfano, endapo dhamana ya mkopo ni mali au hisa, chama kitapaswa kuthaminisha dhamana hizo ili ziendane na mabadiliko ya soko. Aidha, kama dhamana ya mkopo ni bidhaa za mkopaji, chama kitatakiwa kufanya ukaguzi wa bidhaa hizo na kutathmini thamani yake.

e) **Tathminiya nje**

Chama kinatakiwa kushirikiana na taasisi nyingine katika kufanya tathmini ya uwezo wa wakopaji katika urejeshaji wa mikopo. Kwa mfano, mfumo wa upashanaji wa taarifa za wakopaji kwa taasisi za kifedha (*credit referencebureau*).

f) **Mabadiliko yasiyotarajiwa**

Chama kinapaswa kutambua kuwa kuna uwezekano wa kutokea mabadiliko yasiyotarajiwa ambayo yanaweza kuathiri uwezo wa mkopaji kurejesha mkopo wake.

Katikaufuatiliaji waviashiriavilivyotajwahapo juu, chamakitapaswakufuatiliamatumizi ya fedha za mkopo kama zimetumika kwa kuzingatia madhumuni yaliyokusudiwa. Endapo mkopaji atatumia fedha za mkopo kinyume na madhumuni ya mkopo, chama kitapaswa kuainisha hatua za kumchukulia mkopaji huyo.

2.4.6 Dhamana ya mikopo

Vyama hutumia mbinu mbalimbali katika kupunguza vihatarishi vya mikopo. Mbinu hizo ni pamoja na dhamana, wadhamini na kufanya marejesho ya mkopo kupitia amana za wakopaji.

Uwekaji wa dhamana juu ya mikopo iliyotolewa na chama husaidia kupunguza au kuondoa kabisa vihatarishi vinavyoweza kuathiri utoaji wa mikopo katika chama.

Chama kinapaswakuzingatiamamboyafuatayo:

CamScanner

a) Kufanya tathmini ya uwezo wa mkopaji kulipa mkopo na siyo kutumia dhamanakama kigezo cha kutoa mkopo;

b) Ni muhimu kuzingatia masuala ya Kisheria. Nyaraka zote zitakazotumika katika uwekezaji wa dhamana hazina budi kuzingatia masuala ya Kisheria kwa pande zote mbili;

c) ChamakinapaswakuwanaMwongozojuu ya aina zadhamana zinazokubalika;

d) Chama kinapaswa kuhahakikisha kuwa dhamana zinazowekwa ni kamilifu kwa mujibu wa sheria;

e) Chama kinapaswa kuwa na hati za umiliki za dhamana zilizowekwa, kwa mfano hati ya usajili, haki ya kuuza au kubadilisha umiliki na kuhakikisha kuwa zinakidhi matakwa ya Kisheria;

f) Chamakinapaswakuweka taratibuza kufilisidhamanabaadayamuda kukamilika; na

g) Chama kinapaswa kufanya tathmini ya thamani ya dhamana zilizowekwa kila mwaka ili kuangalia kama dhamana hizo bado zina thamani inayotakiwa.

2.4.7 Mfumowa ndani waupimajiwa vihatarishi

Namna bora ya kufuatilia ubora wa mikopo ni kwa kuweka mfumo wa ndani wa upimaji wa vihatarishi. Mfumo mzuri wa ndani wa upimaji wa vihatarishi utawezesha kutofautisha viwango vya vihatarishi vya mikopo vilivyopo kwenye chama. Hii itawezesha kuainisha sifa za mikopo, mikopo yenye matatizo (mikopo mibaya) na utoshelevu wa matengo ya mikopo mibaya.

Mfumo wa ndani wa upimaji wa vihatarishi huainisha mikopo kwenye makundi kwa lengo la kuainisha mikopo iliyopo hatarini. Mfumo wa upimaji wa vihatarishi utaandaliwa kwa kutegemea makundi mbalimbali kutoka katika hali inayoridhisha hadi isiyoridhisha ili kuwezesha kubaini kwa vihatarishi vinavyoweza kujitokeza.

Wakati wa uandaaji wa mfumo wa ndani wa upimaji wa vihatarishi, chama kitatakiwakupima vihatarishi vya mkopo kwa mkopaji pamoja na vihatarishi vya mkopo husika.

Upimaji wa ndani wa vihatarishi ni muhimu katika ufuatiliaji na udhibiti wa vihatarishi vya mikopo. Ili kuwezesha utambuzi wa vihatarishi mapema, mfumo wa ndani wa upimaji wa vihatarishi wa chama unatakiwa kutoa tahadhari ya uwepo au kutokea kwa vihatarishi katika mikopo iliyotolewa, kwa mfano hali ya kifedha na kibiashara ya mkopaji, mwenendo wa mkopaji katika kuzingatia masharti ya mkopo na thamani ya dhamana.

Chama kitatakiwa kuchukua hatua zaidi katika kufuatilia mikopo ambayo ipo katika makundi yasiyoridhisha kwa kuwatembelea wakopaji mara kwa mara na kufanya tathmini ya hali ya mikopo hiyo.

Upimaji wa vihatarishi utasaidia kujua mwenendo wa mikopo iliyotolewa na kuipanga kwenye makundikulingana nahaliya vihatarishi.Upimajiwa marakwa marautasaidiakujua

CamScanner

hali halisi ya mikopo na kusaidia kuhamisha mikopo kutoka katika kundi lisiloridhisha kwenda kwenye kundi linaloridhisha au kutoka katika linaloridhisha kwenda kwenye lisiloridhisha.

2.4.8 Usimamiziwamikopo mibaya

Sera ya mikopo inapaswa kuweka taratibu za kushughulikia mikopo mibaya. Utambuzi wa mikopo mibaya mapema ni muhimu na unarahisisha kuchukua hatua na kudhibiti uwezekano wa kupoteza fedha za chama.

Sera inapaswa kuainisha utaratibu wa kubaini siku ambazo mkopo umecheleweshwa. Sera inapaswa kuainisha taratibu za kuongeza muda wa marejesho, ufutaji wa mikopo na kutoa mikopo ya ziada kwa wakopaji waliopo. Aidha, sera inapaswa kuanisha taratibu za uidhinishaji.

Seraya mikopo inapaswa kuainisha taratibu za ufuatiliaji wamikopo na utoaji wataarifa kwa menejimenti na Bodi ya chama. Sera haina budi kuweka taratibu za uwekaji wa madaraja ya mikopo (*loan classification*) na matengo ya mikopo (*loan provision*).

2.4.9 Miamalakatiya chamanataasisinyingineza kifedha

Miamalakatiyachamana Taasisinyinginezakifedha inawezakusababishavihatarishikatika mikopo. Sera ya miamala kati ya chama na taasisi nyingine za kifedha inapaswa kuainisha mambo yafuatayo:

a) Mipakakati yachamana taasisinyinginezakifedha; na
b) Njiazitakazotumikakufanyamalinganishoyamiamalakatiyachamanataasisi nyingine za kifedha.

2.4.10 Matengonataratibuza kufutamikopomibaya

Sera ya mikopo inapaswa kueleza utaratibu utakaotumika katika kufanya matengo ya mikopo yote. Hii haina budi kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu (… IFRS) pamoja na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha za mwaka 2019.

2.5 Upimajina Ufuatiliajiwa Vihatarishivya Mikopo

2.5.1 Upimajiwa vihatarishivya mikopo

Chama kinapaswa kuweka taratibu za kupima vihatarishi kwenye bidhaa mbalimbali za mikopo ili kukiwezesha kufanya maamuzi sahihi katika kudhibiti vihatarishi.

Upimaji wa vihatarishi unapaswa kuzingatia aina za mikopo inayotolewa, muda wa mikopo, uwepo wa dhamana au wadhamini kwa mikopo iliyotolewa. Chama kitapaswa kufanya tathmini ya uchumi kwa ujumla au sekta fulani ili kuweka mpango wa dharura wa kudhibiti vihatarishi vinavyoweza kujitokeza nje ya chama.

Namna bora ya kufuatilia ubora wa mikopo ni kuweka mfumo wa ndani wa upimaji wa vihatarishi.Mfumo wandani waupimaji vihatarishi ni njianzuri yakutofautishaviwango vya

CamScanner

vihatarishi vya mikopo katika chama. Hii itasaidia katika kuainisha sifa za mikopo, mikopo mibaya na matengo ya mikopo mibaya.

Kwa kawaida, mfumo wa upimaji wa vihatarishi vya mikopo katika chama huainisha sifa za mikopo na kuiweka kwenye makundi. Makundi hayo ni: kundi la kawaida, angalizo, chini ya kiwango, mashaka na hasara.

2.5.2 Usimamizi wa Mikopo

Usimamizi wa mikopo ni muhimu ili kuhakikisha usalama wa mikopo. Ni jukumu la Bodi ya chama kuweka Kitengo cha usimamizi wa mikopo ambacho kitakuwa na jukumu la kusimamia na kufuatilia mikopo yote iliyotolewa na chama. Hii itakuwa ni pamoja nautunzaji wa taarifa za mikopo, kuandaa vigezo na masharti, na ulinzi wa dhamana za mikopo zilizowekwa na wakopaji. Majalada ya mikopo yatapaswa kuwa na taarifa zifuatazo:

i. Maombiyamkopo;

ii. Ushahidiwa idhini;

iii. Taarifazakifedha zahivikaribuni zamkopaji;

iv. Kumbukumbunatareheyakupitia maombiyamikopo;

v. Kumbukumbuzadhamanazamikopo;

vi. Kumbukumbuzavigezonamashartiyamkopo;

vii. UshahidiwadhamanailiyothibitishwanakusajiliwaKisherianautunzajiwake; na

viii. Tathmini yandani(*internalrating*).

Wakati wa kuandaa taratibu za usimamizi wa mikopo, Chama kitapaswa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya chama. Mgawanyo wa majukumu kati ya waidhinishaji wa mikopo na wasimamizi wa mikopo unapaswa kuzingatiwa.

Usimamizi endelevu wa mikopo ni muhimu katika mchakato wa utoaji wa mikopo. Usimamizi wa mikopo ni kazi inayofanywa ili kusaidia kudhibiti utoaji na ufuatiliaji wa mikopo. Kitengo kinachofanya kazi ya usimamizi wa mikopo kitakuwa na majukumu yafuatayo:

a) ***Utunzaji wa kumbukumbu:*** Kuhakikisha nyaraka zote muhimu zinazohusiana na mikopo zimekamilika (mikataba ya mkopo, dhamana, wadhamini) kulingana na vigezo na masharti yaliyopo. Nyaraka ambazo hazijawasilishwa zinapaswa kufuatiliwa;

b) ***Utoaji wa mikopo:*** Kitengo cha usimamizi wa mikopo kinapaswa kuhakikisha kwamba mikopo iliyotolewa imeidhinishwa. Mikopo itolewe baada yakusainiwa kwa mikataba ya mikopo na kuwasilishwa kwa hati ya dhamana za mikopo kama ni zaidi ya akiba na amana zilizopo chamani;

CamScanner

c) *Ufuatiliaji wa mikopo:*Mara baada ya mkopo kuidhinishwa na kutolewa, utatakiwa kufuatiliwa. Hii ni pamoja na kumfuatilia mkopaji ili kuhakikisha kwamba anatekeleza masharti ya mkataba; kuainisha dalili za ukiukwaji wa masharti; kufanya uthaminishaji wa dhamana za mikopo mara kwa mara na ufuatiliaji wa marejesho kwa wakati;

d) *Marejesho ya mikopo:* Wakopaji wanatakiwa kufahamishwa muda na wakati ambao watatakiwa kufanya marejesho ya mikopo yao. Endapo mkopaji atashindwa kurejesha mkopo au atachelewa kufanya marejesho, atatakiwa kutoa taarifa kwa uongozi wa chama. Chama kinapaswa kutunza kumbukumbu sahihi mara baada ya kupokea marejesho ya mkopo;

e) *Utunzaji wa majalada ya mikopo*: Chama kinapaswa kuweka mwongozo wa utunzaji wa majalada ya mikopo. Majalada ya mikopo hayapaswi kuwa na mawasiliano ya mkopaji tu bali pia taarifa za kifedha za mkopaji na taarifa za marejesho ya mikopo; na

f) *Nyaraka za Dhamana:* Chama kinapaswa kuhakikisha kuwa nyaraka zote za dhamana zinatunzwa sehemu salama ambayo haziwezi kuharibiwa kwa mfano kuungua moto, kuibiwa, n.k. Aidha, chama kinatakiwa kuwa na daftari la usajili wa dhamana na udhibiti wa nyaraka hizo;

Chama kinapaswa kuwa na utaratibu wa kufuatilia na kutathmini bima za mikopo audhamana za mikopo iliyotolewa. Aidha, chama kitapaswa kufanya uhakiki wa usalama wa nyaraka mara kwa mara.

Kwa upande wa Vyama vidogo ambavyo vitashindwa kuwa na kitengo cha usimamizi wa mikopo kwa kushindwa kumudu gharama, vinatakiwa kuwa na mtu mmoja ambaye atashughulikia masuala ya mikopo kama vile utunzaji nyaraka za mikopo, kutoa mikopo, ufuatiliaji wa wakopaji na kutoa taarifa kwa Meneja wa chama.

2.5.3 UtoajiwaTaarifazaVihatarishi

Taarifa za vihatarishi vya mikopo zinatakiwa kutolewa kwenye Bodi na Menejimenti ya chama. Taarifa hizo zinatakiwa kuwa na uhalisia na kutolewa kwa wakati. Aidha, taarifa hizo zinatakiwa ziwe zinahusu shughuli za mikopo, kwa mfano:

a) Vihatarishikatikabiashara,bidhaanasekta kwaujumla;

b) Vihatarishi vinavyotokana na wadau kama vile wateja binafsi, makampuni na taasisi nyingine za kifedha;

c) Vihatarishivinavyohusiananawakopajiwakubwa,wakopajiwenyemahusianoau vikundi vya wakopaji;

d) Mikopo mibaya kwa kuzingatia aina ya mikopo husika ikionesha kiasi kilichocheleweshwa;

e) Mikopomibayailiyobadilishiwamasharti kwakipindi fulani;

CamScanner

2.5.4 Mfumo wausimamiziwataarifa

Chama kinapaswa kuwa na mfumo wa usimamizi wa taarifa ambao utawezesha Bodi na Menejimenti ya chama kupata taarifa za uhakika ambazo zitaisaidia kuchukua hatua katika kudhibiti vihatarishi vya mikopo. Mfumo huo unatakiwa:

a) Kuruhusu kufanyika kwa tathimini ya mikopokwa mfano, mfumo unatakiwa kutoa mchanganuo wamikopo kwa aina, muda, mahali/eneo analoishi mkopaji, aina ya dhamana au taarifa nyingine yoyote kulingana na mahitaji ya chama;

b) Kufafanua masharti ya mkopo (viwango vya riba, ratiba ya marejesho, aina ya dhamana au mdhamini) na kutoa taarifa ya marejesho ya mkopo;

c) Kuruhusu kuunganishwa kwa mikopo kwa kuzingatia wateja, sekta, eneo lakijiografia au muda ili kuwezesha kufanyika kwa uchambuzi wa mikopo;

d) Kuruhusukuainishavihatarishikatika mikopo;

e) Kuwezesha kupanga mikopo katika makundi ili kusaidia kuanisha kiwango cha matengo kinachotakiwa kwa kila kundi na mikopo yote kwa ujumla;

f) Kutoa taarifa ya mapato ya riba ambayo haijakusanywa kutokana na mikopo ambayo haijarejeshwa; na

g) Kutoataarifazaakauntizamikopoambazomiamalahaijakamilika.

2.6 Udhibiti wa Ndani na Ukaguzi

Chama kinapaswa kuwa na mfumo huru wa udhibiti wa ndani kwa ajili ya kufanya tathmini ya hali ya vihatarishi vya mikopo ili kuisaidia Bodi ya chama kujua kama mfumo wa udhibiti wa vihatarishi vya mikopo unafanya kazi ipasavyo.

Matokeo ya ukaguzi yanatakiwa kuwasilishwa kwenye Bodi na Menejimenti ya chama. Ukaguzi unatakiwa kutoa taarifa sahihi ambazo zitaiwezesha Bodi na Menejimenti ya chama kufanya tathmini ya hali ya mikopo.

Mapitio ya mchakato wa utoaji wa mikopo unapaswa kujumuisha uchambuzi wa miongozo mbalimbali itakayotumiwa katika utoaji wa mikopo pamoja na kupitia hatua za uombaji, tathmini, uidhinishwaji, ufuatiliaji, ukusanyaji na udhibiti wa mikopo.

Timuyaukaguzi wandani inapaswa kuhakikishayafuatayo:

a) Taratibuzautoaji wamikopo zinafuatwa;

b) Vihatarishi vya mikopo vipo katika viwango vinavyokubalika Kisheria na mipaka iliyowekwa na Bodi ya chama;

c) Uidhinishaji wa mabadiliko makubwa katika mchakato wa/taratibu za usimamizi wa vihatarishi;

d) Kuwepo kwa uhakiki endelevu wa taarifa sahihi zinazotumiwa kwenye mfumo wa ndani wa upimaji vihatarishi;

CamScanner

e) Serayamikopo nataratibu zautoaji wamikopo zinazingatiwa;

f) Mfumowandani waupimajiwavihatarishi unazingatiwa; na

g) Uanishwajiwamaeneoyenyemapungufukwenyeusimamiziwa vihatarishi.

Ukaguzi wa ndani unapaswa kufanywa angalau mara nne kwa mwaka. Ukaguzi wa ndani unatakiwa kuainisha maeneo dhaifu katika usimamizi wa vihatarishi pamoja na kubaini udhaifu katika mchakato wa usimamizi wa hatari na upungufu uliopo kwenye sera na taratibu za usimamizi wa mikopo.

SEHEMU YA TATU

KIHATARISHICHAMKAKATI

3.1 Utangulizi

Kihatarishi hiki kinatokana na chama kushindwa kutekeleza ipasavyo mpango biashara, mpango mkakati na kwa ujumla kutakuwa na maamuzi sahihi katika mgawanyo warasilimali,nakutoendana namabadilikoyamazingirayakibiashara nahatimayekupataathari kwenye Mapato na au mtaji.

Vihatarishivinawezakutokanana:

a) Kutolinganakwamkakati namalengo yachama;

b) Kutoandaliwa kwa Mkakati wa mpango wa maendeleo na hivyo kushindwa kufikiamalengo ya chama;

c) Kutokuweponarasilimalikwaajiliyakufanyia biashara;

d) Rasilimali kutotumikakwakuzingatiamalengoyachama; na

e) Utekelezajiwashughulizachama usiozingatiaubora.

3.2 Vyanzovya Ujumla vyaVihatarishi vya Kimkakati

Vihatarishi vya Kimkakati vinaweza kutokea kwa njia mbalimbali kutegemeana na mazingira ya chama husika. Vyanzo vya ujumla vya vihatarishi hivyo ni kama vifuatavyo:

a) Ushindani – kuingia kwa wafanyabiashara na bidhaa mpya zinazoshabihiana na zileza SACCOS;

b) Teknolojia–mabadilikoyakitekinolojia;

c) Kutegemeakufanyabiasharana wanachamawachache;

d) Sababu za kiuchumi kama vile kupanda au kushuka kwa hali ya maisha, mabadilikoya gharama za fedha, n.k.;

e) MabadilikoyaSheria;

f) Kutokuwanautaratibu mzuriwakufanyakazi;

g) Kutokuwanautaratibumzuri wautoaji taarifanakufanyikakwamaamuzi;na

h) Kushindwa kudhibiti uwekezaji katika shughuli nyinginezo nje ya madhumuni makuu ya chama, kwa mfano; Ardhi na Majengo.

3.3 Wajibu wa Bodina Menejimenti

Wajumbe wa Bodi na Menejimenti ya chama ni muhimu sana katika kusimamia mfumoimara wa kudhibiti vihatarishi vya kimkakati. Bodi inawajibika kudhibiti vihatarishi vya kimkakati ikiwa ni pamoja na kuweka mpango mkakati wa kudhibiti vihatarishi kwa Chama nakufanyamapitioyautekelezajiwake.Menejimentiinajukumulakuhakikishakuwa

kunakuwepo na mkakati thabiti wa kudhibiti vihatarishi vya kimkakati ambao utatekelezwaili kuleta mwelekeo wa maono ya Bodi kupitia sera mbalimbali za chama.

Ili kufanikisha hilo, Menejimenti ya chama inatakiwa kutambua aina/asili na ngazi ya vihatarishi vinavyohusiana na utekelezaji wa mpango mkakati wa chama na jinsi gani vihatarishi hivyo vinaweza kuathiri utekelezaji wa mkakati wa biashara ndani ya chama.

3.3.1 Wajibuwa Bodikatikakudhibiti Vihatarishi

Wajibuwawajumbewa Bodi katika kusimamiavihatarishi vyakimkakati ni pamoja na:

a) Kuweka malengo ya Chama, misingi ya maadili na maono ya chama ili kuhakikisha kuwa yanatekelezwa kikamilifu na kwa ufanisi katika ngazi zote za chama;

b) Kuhakikishakuwa utekelezaji wamwongozo waudhibiti wavihatarishi unaendana na mpango mkakati wa chama; na

c) Kuhakikisha kuwa mfumo mzima wa utambuzi na udhibiti wa vihatarishi vya kimkakatiunasimamiwaipasavyokatikangazizotena unalingananampango mkakati wa maendeleo ya biashara.

3.3.2 Wajibu wa menejimenti

Menejimentiyachamaitakuwanamajukumu yafuatayo:

a) Kuanzisha na kutekeleza mfumo wa usimamizi na udhibiti wa vihatarishi vya kimkakati kwa kuzingatia vigezo na viwango vilivyowekwa na Bodi;

b) Kusaidia Bodi katika kutengeneza mikakati ya maendeleo ili kukidhi malengomahsusi ya kimkakati na malengo ya jumla ya chama;

c) Kuwekampango wautekelezajiwampangomkakatiwachama;

d) Kuhakikisha kwamba mpango mkakati uliopitishwa na kuidhinishwa unatekelezwa kwa ufanisi;

e) Kutekelezakwaufanisimfumowatathmini yamatokeo yashughulizachama; na

f) Kuhakikisha kwamba mambo ya kimkakati na vihatarishi muhimu vinavyotokana na mabadiliko ya kimazingira au utekelezaji wa mpango mkakati wa chama vinatolewa taarifa kwa Bodi mara kwa mara na kwa wakati.

3.4 Sera,TaratibunaUkomo

3.4.1 Mchakatowa mpangomkakati

Utengenezaji wa mpango mkakati wa chama usio na viwango vinavyokubalika unasababisha Chama kuwa katika hali ya hatari katika utekelezaji wa mpango huo. Kila chama kinatakiwa kuandaa mpango mkakati unaojitosheleza ambao utakwenda sambamba na makisio yamapato na matumizi. Mpango mkakati utasaidia kuainisha malengo mahsusi ya vipaumbelena njia bora zinazowezesha kufikia malengo yaliyowekwa kwa mujibu wa vipaumbele.

CamScanner

Kilachamakinatakiwakuzingatiaushirikishwajikatikangazizote.Ilikuwanampango mkakati mahsusi na unaotekelezeka, unatakiwa kuzingatia yafuatayo:

a) UwezeshajinaushirikishwajiwaBodi, kamatimbalimbalinamenejimentiyachama;

b) Utoshelevu wa taarifa zitakazosaidia uchambuzi wa masuala ya kiuchumi, hali ya chama ukilinganisha na washindani, hali halisi ya masoko, mahitaji ya wanachama na mengineyo;

c) Uthabiti *(consistency)* wa mpango wa uendeshaji kwa kulinganisha na mkakati na malengo ya chama; na

d) Upimaji wa matokeo ya mpango mkakati kwa kuangalia hali halisi ya utekelezaji ukilinganisha na mpango mkakati uliopita.

3.4.2 Mamboyakuzingatiakatika uandaajiwampango mkakati

Bodiyachamainatakiwakuhakikishamamboyafuatayoyanazingatiwakatikakuandaampango Mkakati wa kudhibiti vihatarishi:

a) Malengonamadhumuniyachama;

b) Uchambuzi wa masuala ya kiuchumi, kijamii, kiteknolojia na mazingira ya ushindani yanayohusiana na chama;

c) Mahitajiyawanachamapamojanabidhaazitolewazochamani;

d) Tathminiyakina kuhusiananamfumo wabiasharainayofanyikaikiwani pamoja na;

- Tathminikuhusumapatonamatumizipamojanahaliyafedhakatika chama,
- Wanachama na fungamano la pamoja, uwezo wa ushindani na mpangiliowa masuala ya kiutawala, na
- Udhibitiwavihatarishi nauwezowa kiutendaji;

e) Kuwa na tathmini huru ya mkaguzi wa nje, mapitio ya uendeshaji, taarifa ya mkaguzi wa ndani, taarifa za ukaguzi wa wasimamizi (kutoka Tume) na taarifa nyinginezo kutoka kwa wadau;

f) Kuwa na mfumo wa usimamizi unaojumuisha usimamizi kwa mujibu wa matakwa ya kisheria pamoja na mwongozo wa utekelezaji;

g) Kuwepokwaukomowauhimilivu wavihatarishi katika uendeshajiwachama; na

h) Tathmini ya rasilimali fedha na zisizo za kifedha zinazohitajika katika kuwezesha shughuli zinazofanyika au zitakazofanyika katika utekelezaji wa mpango mkakati. Tathmini inatakiwa kuzingatia aina, wigo na ugumu wa taarifa za vihatarishi zilizopo chamani.

CamScanner

3.5 MamboyaMsingiYanayotakiwaKuwemo kwenyeMpangoMkakati

Mpango mkakati wa chama ulioidhinishwa na Bodi unatakiwa kuwa na angalau mambo yafuatayo:

a) Malengoyashughuli za chama kwakipindi kisichopunguamiakamitatu (3);

b) Ainanamawandayashughulizinazofanywanachama;

c) Mbinunaserazitakazotumikakatikakufanikisha malengoyachama;

d) Shabahanavigezo vyatathmini katika kufikiamalengo yachama;

e) Makisio ya kifedha ya chama kwa kipindi cha miaka mitatu yakijumuisha tathmini na uchambuzi wa kifedha;

f) Mpango wa kupata vyanzo vya fedha ili kuwezesha makisio ya Mapato na matumizi; na

g) Uendelevuwachama kwakuzingatia ushindani uliopo.

3.6 MpangiliowaMabadilikokatikaMenejimenti

Kablayakuanzautekelezaji wamkakati, chamakinatakiwakuhakikishakuwakunarasilimali za ndani za kutosha na utaratibu wa kuhakikisha kuwa malengo yaliyowekwa yanafikiwa na kwamba upo ushirikiano miongoni mwa Idara mbalimbali ambao utarahisisha uwajibikaji wakati wa utekelezaji.

Mpangilio wa utekelezaji utafanyika kwa kuhakikisha kwamba mchakato wa matumizi ya rasilimali za ndani unazingatia yafuatayo:

- Uwepowarasilimalizakutoshazitakazogawanywakatikakutekeleza majukumu ya msingi;
- Kuwekawatusahihikatikanafasisahihi; na
- Kuwekamuundonausimamiziwavihatarishi,mifumo,miundombinunateknolojia unaoweza kusaidia katika kupokea mabadiliko mapya.

3.7 Michakatomingineya Kusaidia

3.7.1 Mpangowa usimamiziwa mahitajiya fedha

Chama kitatenga rasilimali za kutosha kwa kuzingatia shughuli zinazotekelezwa kwa mujibu wa mpango mkakati.

3.7.2 Usimamiziwa mifumoya Tehama

Kulingana na mazingira ya ushindani wa utoaji wa huduma za kifedha, uwezo katika utunzaji wa taarifa ni muhimu kwa chama ili kutoa fursa ya ushindani, ubunifu wa bidhaa na huduma mpya katika kufikia malengo. Chama kinatakiwa kuwa na mfumo wa habari na mawasiliano imara na thabiti kwa ajili ya utekelezaji wa mpango mkakati na mchakato wa kufanya maamuzi ndani ya chama.

CamScanner

3.7.3 UsimamizinamaendeleoyaRasilimaliWatu

Usimamizi wa Rasilimali Watu ndani ya chama utazingatia mtazamo wa kimkakati ambao unajumuisha uwajibikaji katika kufanikisha malengo na kutengeneza utamaduni na miiko yake.

3.7.4 Mpangowaurithishaji(*successionplanning*)

Chama kinatakiwa kuandaa mpango wa urithishaji ili kukabiliana na changamoto za watumishi kuacha kazi, kuhama au kustaafu. Mpango wa urithishaji wa madaraka kwa watumishi ni wa muhimu hasa katika ngazi za juu na za kati za uongozi ili kuziba mapengo kutokana na kuacha kazi, kuhama au kustaafu. Bodi ya chama inatakiwa kuandaa utaratibuwa mpango wa urithishaji madaraka, hususan kwenye nafasi ya watendaji wakuu, wa chama.

3.8 Upimaji naUfuatiliaji

Kufanikiwa au kutofanikiwa kwa mkakati wa chama kunategemea rasilimali na uwezo wa utekelezaji wa mpango mkakati pamoja na uwezo wa kupima, kudhibiti na kufuatilia maendeleo ya utekelezaji wa mpango huo. Bodi na Menejimenti ya chama, kwa kuzingatia vihatarishi vya kimkakati, watahakikisha uwepo wa umakini katika udhibiti wa utekelezajiwa mkakati.

Chama kinatakiwa kuwa na mwongozo mahsusi na taratibu zilizoainishwa za ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkakati, na utoaji wa taarifa za utekelezaji. Chama kinapobaini matokeo yasiyotarajiwa kutokana na uendeshaji, mabadiliko ya soko ambayo yanaweza kuathiri biasharaauhaliyafedha,matokeohayoyanatakiwakutolewataarifamaramojakwenyeBodi na Menejimenti ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa wakati.

Ili kuhakikisha kuwa kunakuwepo na mfumo imara wa udhibiti wa vihatarishi, kila chama kinatakiwa kuwa na utaratibu mahsusi wa mfumo wa mawasiliano unaowezesha ufuatiliaji taarifa mbalimbali kama ifuatavyo:

a. Haliyakiuchumiyasasanayabaadae;kwamfano,ukuajiwauchumi, mfumuko wa bei, riba, mabadiliko ya mwelekeo (*trend*) n.k;

b. Haliyasasana yabaadaeyakisekta nahali yamasokokama;

- Kuongezekakwaushindani kutokananamasokomapya,
- Kubadilikakwatabia/mahitajiya wanachama,
- IdadiyaVyama vilivyoungana,
- Bidhaampya, n.k.;

c. Mabadilikokatikasektambalimbalikwakuzingatiavihatarishivyakisekta, mfano, kilimo, n.k.

Kulinganisha matokeo halisi na matokeo yaliyotarajiwa ni nyenzo muhimu ya upimaji wa utekelezaji wa mpango mkakati na unatoa mwanya kwa uongozi kuchukua hatua za haraka katikakutatuatatizonakurekebishatofautizilizobainishwakulingananamalengotarajiwa.

CamScanner

Hivyo, chama kinatarajiwa kuandaa mfumo/mpango wa ufuatiliaji utakaosaidia kupima malengo.

Kuwepo na mwendelezo wa kufanya tathmini na kuweka malengo ya kimkakati yanayopimika ya muda mrefu pamoja na shabaha zinazotakiwa kugawanywa katika kipindi cha muda mfupi (angalau mwaka mmoja).

3.9 Udhibiti wa ndaninaUkaguzi

Bodi na Menejimenti ya chama zinatakiwa kuwa na mfumo thabiti wa udhibiti wa ndani ili kuhakikisha kuwa vihatarishi vya kimkakati vinadhibitiwa ipasavyo. Mfumo wa udhibiti wa ndani utahakikisha kuwa:

a) Muundo wa kiutawala wa chama unabainisha mamlaka ya uwajibikaji katika kila ngazi;

b) Mfumonamuundo wachama unaruhusuukuaji nauendelevuwabiashara;na

c) Mchakato wa kupanga na kufanya mapitio ya mpango mkakati wa chama ni wa kina na unafuatwa.

Matokeo ya mapitio ya ukaguzi yaliyojumuisha mambo mbalimbali na upungufu uliobainika yatatolewa taarifa kwenye Bodi na Menejimenti ya chama. Bodi na Menejimentiwatawajibika kutoa ushirikiano kwa mkaguzi wakati wa mapitio ili kusaidia kudhibiti vihatarishi vya kimkakati na kuainisha mambo muhimu ambayo yanapaswa kushughulikiwa ipasavyo.

SEHEMUYANNE

USIMAMIZIWAKIHATARISHICHA UENDESHAJI

4.1 Utangulizi

Kihatarishi cha Uendeshaji ni upungufu unaotokana na muundo wa kiuendeshaji katika udhibiti wa ndani, watendaji wa chama, mfumo wa usimamizi wa taarifa au matukio ya nje yanayojumuisha vihatarishi vya kisheria. Chama kinatakiwa kufuata mwongozo huu na kuweka usimamizi madhubuti wavihatarishi vya uendeshaji unaokidhi hali halisi, viwango na changamoto za kuzuia vihatarishi vya uendeshaji. Mfumo huu unatakiwa kujumuisha angalau vipengele vifuatavyo:

a) Uangalizinaudhibiti kupitia Bodiya chama;

b) Majukumunauwajibikaji waMenejimenti yachama;

c) Muundo sahihi/madhubuti wachama;

d) Seranataratibuzausimamiziwavihatarishivya uendeshaji; na

e) Mapitiohuru(*independentreview*).

4.2 Wajibu wa Bodina Menejimenti

4.2.1 Wajibu wa Bodi

Katikakusimamia vihatarishi vya uendeshaji, Bodiinamajukumu yafuatayo:

a) Kuandaa mfumo wa utawala utakaowezesha kuelewa aina na wigo wa vihatarishi vya uendeshaji na jinsi ya kuviepuka;

b) Kushirikiana na Menejimenti katika kuandaa mikakati na sera mbalimbali kuhusiana na vihatarishi vya uendeshaji;

c) Kutathmini na kuidhinisha shughuli za usimamizi, na kutoa taarifa za mipango ya usimamizi wa vihatarishi vya uendeshaji ili kuhakikisha kuwa ufanisi unakuwepo katika mfumo wa maamuzi ndani ya chama;

d) Kuhakikisha kuwa Menejimenti inatumia njia sahihi katika kutambua, kutathmini, kufuatilia na kudhibiti vihatarishi vya uendeshaji kwa kuzingatia viwango bora;

e) Kuhakikisha kuwa kunakuwepo utaratibu mzuri wa kupongeza au kutoa adhabu ili kuwezesha kusaidia maendeleo ya utekelezaji wa mfumo wa vihatarishi vya uendeshaji;

f) Kupitia mara kwa mara taarifa za usimamizi wa vihatarishi vya utendaji zinazowasilishwa na Menejimenti; na

g) Kuhakikisha kuwa vihatarishi vya uendeshaji ndani ya chama vinakaguliwa ipasavyo kupitia wakaguzi wa ndani au ikiwezekana mtu huru wa nje atakayefanya mapitio.

CamScanner

4.2.2 Wajibu wa Menejimenti

Menejimenti ya chama ina jukumu la kusimamiavihatarishi vya uendeshaji. Majukumu hayo ni pamoja na:

a) Usimamiziwavihatarishi vyauendeshaji wakilasiku;

b) Kutekeleza na kupitia mara kwa mara sera na hatua za usimamizi wa vihatarishi vya uendeshaji, mikakati na sera zote kwa ujumla zilizopitishwa na kuidhinishwa naBodi;

c) Kufanya upembuzi yakinifu na kuielewa kwa ujumla hali ya chama katika usimamizi wa vihatarishi vya uendeshaji;

d) Kufafanua kwa uwazi wajibu wa kila Idara kwa kuzingatia shughuli za usimamizi wa vihatarishi vya uendeshaji pamoja na utoaji wa taarifa za mara kwa mara;

e) Kuwezesha usimamizi wa vihatarishi vya uendeshaji kwa kuwa na Rasilimali za kutosha kuwezesha kuwa na miundo inayojitosheleza, mafunzo kwa watumishi wanaohusika na vihatarishi vya uendeshaji; na

f) Kutoataarifa zamarakwamara kwaBodi yachamakuhusu usimamizi wavihatarishi vya uendeshaji.

4.3 SeranaUtaratibu waUsimamiziwaVihatarishivya Uendeshaji.

Chama kinaweza kuingia kwenye vihatarishi vya uendeshaji kinapokuwa kimeingia kwenye biashara au uanzishaji wa bidhaa mpya au mifumo ya teknolojia. Chama hakina budi kuhakikisha kuwa ipo miundombinu sahihi katika kusaidia ukuaji au kupokea mabadiliko ya bidhaana mifumo. Ni muhimu kwachama kuwa na sera na taratibu zitakazoelekeza utaratibu wa kufanya mapitio ya kuidhinisha bidhaa mpya, shughuli mbalimbali pamoja na mifumo. Yafuatayo ni muhimu yazingatiwe:

a) Kuzingatiavihatarishi vinavyoambatanana bidhaa,shughuli au huduma mpya;

b) Uhimilivu wa mabadiliko katika vihatarishi vya uendeshaji kwa kuzingatia aina ya bidhaa na shughuli za chama;

c) Udhibiti katika mchakato wa menejimenti ya vihatarishi pamoja na mkakati wa kuviepuka;

d) Mabadilikoyavihatarishihusikakwamujibuwakiwangokilichowekwa;na

e) Utaratibu mpya wa upimaji na ufuatiliaji wa vihatarishi katika shughuli na bidhaa mpya.

4.4 Upimaji,Ufuatiliaji naUdhibitiwaVihatarishi

4.4.1 Upimaji

Njiazinazowezakutumika katikakupimavihatarishivyauendeshajinikamaifuatavyo:

a) Matokeo ya ukaguzi wa ndani na nje: Matokeo ya ukaguzi huo kimsingi yatasaidia katika kuzuia upungufu uliojitokeza kwenye taarifa hizo;

b) Upotevu wa taarifa: Takwimu hizo zitasaidia kujua hali ya chama katika vihatarishi vinavyotokea na mwelekeo wa udhibiti wa ndani;

c) Ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za nje: Takwimu za nje zinasaidia chama katika kujua mwelekeo wa matokeo ya hasara zinazoweza kujitokeza katika sekta ya SACCOS. Takwimu hizi za hasara zilizooneshwa ndani na nje zinaweza kulinganishwa na kusaidia katika kujua udhaifu na kufanya maboresho ili kuepukana na vihatarishi husika;

d) Kufanya tathmini ya vihatarishi: Tathmini hii itasaidia chama kujua matokeo hasi au chanya kwa ajili kufanya maamuzi;

e) Kupima mwelekeo wa biashara: Mwelekeo wa biashara husaidia kuainisha hatua za kuchukua katika kuepukana na vihatarishi na pia kupanga vipaumbele katika kufanya maamuzi na kuepukana na vihatarishi;

f) Viashiria vya kiutendaji: Husaidia kuonesha mwelekeo wa viwango vya vihatarishi katika chama; na

g) Upimaji wa vihatarishi: chama kikubwa kinaweza kuangalia vihatarishi vyauendeshaji kwa kutumia matokeo ya tathmini ya vihatarishi pamoja na makadirio ya vihatarishi husika.

4.4.2 Ufuatiliaji

Chama kinapaswa kuweka utaratibu wa kufanya ufuatiliaji wa vihatarishi vya uendeshaji na hasara zinazoweza kujitokeza, pamoja na kutoa taarifa muhimu kwenye Bodi kwa lengo la kuchukua hatua za haraka za usimamizi wa vihatarishi vya uendeshaji.

Mfumo thabiti wa ufuatiliaji ni muhimu kwa ajili ya kusimamia vihatarishi vya uendeshaji. Ufuatiliaji wa mara kwa mara wa vihatarishi unaweza kusaidia kubaini kwa haraka na kuboresha upungufu uliopo kwenye Sera, Mikakati na taratibu za kusimamia vihatarishi vya uendeshaji. Utambuzi wa haraka wa vihatarishi hivyo unaweza kusaidia kupunguza matukio ya hasara yanayoweza kujitokeza chamani.

Vile vile, katika kudhibiti utendaji hasi wa chama. Chama kinapaswa kubaini mapema viashiria vinavyotoa ishara ya kuongezeka na kusababisha hasara chamani. Viashiria hivyo vinapaswa kuangaliwa katika ufanisi wa mbeleni chamani na lazima vihusishe vyanzo muhimu vya vihatarishi hivyo vya uendeshaji, kwa mfano: ukuaji wa haraka, uanzishaji wa bidhaa mpya, kuacha kazi kwa watumishi, kupungua kwa miamala, kusimama kwa mifumo yauendeshajinamengineyo.Ukomowavihatarishiunapohusishwanaviashiriahivi,

CamScanner

ufuatiliaji wa haraka unaweza kusaidia kubaini vihatarishi kwa uwazi na kuwezesha chama kuchukua hatua stahiki kwa wakati.

Ufuatiliaji wa vihatarishi unapaswa kuwa sehemu ya shughuli za chama na taarifa yake ya Menejimenti inapaswa kuwasilishwa kwenye Bodi ya chama. Matokeo ya shughuli za ufuatiliaji yanatakiwa kujumuishwa mara kwa mara katika taarifa ya Menejimenti pamoja na Bodi ya chama kwa kupitia matokeo ya ukaguzi wa ndani na usimamizi wa kazi zavihatarishi.

Menejimenti inapaswa kupokea taarifa za mara kwa mara kutoka sehemu muhimu ndani ya chama kama kitengo cha biashara, kazi za jumla, ofisi ya usimamizi wa vihatarishi na mkaguzi wandani. Taarifayausimamizi wavihatarishi inapaswakujumuishataarifayandani ya fedha, uendeshaji na takwimu za utekelezaji wa Sheria pamoja na taarifa za nje za masoko juu ya matukio na mazingira ambayo ni muhimu kuangaliwa kwa ajili ya kufanya maamuzi. Taarifa ni lazima isambazwe kwenye Menejimenti na kwenye maeneo muhimu ya chama ambayo yanaweza kuwa na athari.

Taarifa haina budi kuonesha eneo lolote lililobainishwa kuwa na matatizo na utaratibu wa kuchukua hatua za haraka kwa ajili ya kufanyia kazi mambo yaliyobainishwa. Ili kuhakikisha kuwa taarifa hii ya vihatarishi na taarifa ya ukaguzi inatumika na kurejewa, Menejimenti inapaswa mara kwa mara kuonesha muda, usahihi na umuhimu wa mfumo wa utoaji wa taarifa na udhibiti wa ndani kwa ujumla.

Menejimenti kuu pia inaweza kutumia taarifa iliyoandaliwa na vyanzo vya nje (Wakaguzi na Wasimamizi) katika kutathmini manufaa na uhakika wa taarifa za ndani. Taarifa zinapaswa kupitiwa na kuchambuliwa kwa mtazamo wa kuboresha utendaji kazi wa Mwongozo wa usimamizi wa vihatarishi uliopo na kuandaa Sera na taratibu mpya za usimamizi wa vihatarishi chamani.

Kwa ujumla, Bodi inapaswa kupokea taarifa za kutosha juu ya vihatarishi ili waweze kufahamu kwa ujumla mazingira ya usimamizi wa vihatarishi husika, na hivyo kuelewa vihatarishi vya uendeshaji na kujikita katika masuala ya msingi ya kimkakati kwa ajili ya maboresho na kukabiliana na vihatarishi vya kibiashara.

4.4.3 Udhibitina kukabiliana na vihatarishi

Bodi na uongozi wa chama wanatakiwa kuandaa sera, hatua na utaratibu wa kudhibiti vihatarishi vya kiutendaji kama vilivyoainishwa. Chama kitatakiwa kuwa na mfumo wa kuhakikisha kwamba vigezo vinazingatiwa katika mazingira ya kutii matakwa ya Sheria, Kanuni na taratibu pamoja na sera za ndani zinazojumuisha mifumo ya vihatarishi vya uendeshaji.

Usimamizi wa vihatarishi unapaswa kulingana na ukuaji na mabadiliko ya shughuli za biashara; kwa mfano, bidhaa mpya na kuingia katika masoko mapya.

Kipengele muhimu katika udhibiti wa vihatarishi vya uendeshaji, ni uwepo wa mfumo thabiti wandaniambaoutasaidiauongozikatikamfumowaudhibitiwandani.Aidha,mfumowa

CamScanner

udhibiti wa ndani unapokuwa umeandaliwa na kuimarishwa vizuri, utakiwezesha chama kupunguza uwezekano wa makosa ya kibinadamu na upungufu mbalimbali ambao utasaidia katika ugunduaji wa matatizo mapema iwezekanavyo pale yanapojitokeza.

(a) Chama kinatakiwa kuwa na mfumo madhubuti wa udhibiti wa ndani ambao utahakikisha kuwa:

i. Mgawanyo stahiki wa majukumu, na mtumishi asipewe majukumu yatakayosababisha mgongano wa kimaslahi;
ii. Ufuatiliajiwakaribunauzingatiwajiwaviwango vyavihatarishinauchunguzi wa ukiukwaji;
iii. Kuendelea kulinda upatikanaji na utumiaji wa mali na utunzaji mzuri wa kumbukumbu za chama;
iv. Watumishikuwana ujuzinakupatiwamafunzo mbalimbali;
v. Kutambua nyanja au fursa za biashara au bidhaa kwa mujibu wa matokeo tarajiwa; na
vi. Uhakikiwamara kwamaranakufanya malinganisho ya miamalaya hesabu.

(b) Chama kinatakiwa kupunguza vihatarishi kwa mujibu wa vihatarishi vya uendeshaji. Aidha, uangalifu unatakiwa kuchukuliwa ili kupunguza uwezekano wa kupoteza fedha za chama kwa matukio ambayo yatasababisha vihatarishi visivyoepukika.

(c) Chama kinatakiwa kutumia udhibiti wa vihatarishi kama njia ya kujikinga, katika kuzuia vihatarishi vya uendeshaji. Uangalifu unapaswa kuchukuliwa katika kupunguzavihatarishi kwanjia yakukataBima, kuhamishavihatarishi kwakuanzisha biashara nyingine au eneo jingine.

(d) Chama kinatakiwa kuwa na sera husika na utaratibu madhubuti wa kudhibitivihatarishi vinavyotokana na uendeshaji kama ifuatavyo:

i. Shughuli nabidhaampya;
ii. Mabadiliko ya mifumo ya Teknolojia ya habari na Mawasiliano (TEHAMA), vifaa na vitendea kazi.
iii. Hudumazakielektroniki naSimu benki.
iv. Mipangilio ya utumiaji;
v. Utakatishajiwa fedha;
vi. Uhakika/uhaiwa wanachama;na
vii. Nyarakazanjekama mikatabanataarifazamiamala.

4.5 Udhibiti wa ndanina ukaguzi

Idara ya ukaguzi wa ndani katika chama, haitahusika moja kwa moja katika utekelezaji wa mpango mkakati wa vihatarishi vya uendeshaji kutoka katika idara nyingine, bali, itakuwa inahusika katika kuangalia na kufanya tathmini ya mara kwa mara ya jinsi chama kinavyotekelezampangohuo;kusimamiautekelezajiwaseranataratibuzaudhibitiwa

CamScanner

usimamizi wa vihatarishi vya uendeshaji, mikakati na taratibu maalum zilizowekwa na Bodi ya chama katika kupokea taarifa za tathmini ya matokeo ya vihatarishi vya uendeshaji na mifumo ya usimamizi.

SEHEMUYATANO

USIMAMIZIWAVIHATARISHIVYATEKNOLOJIAYAHABARI NA MAWASILIANO

5.1 Utangulizi

Ukuaji wa chama unategemea sana Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kutoa huduma kwa wanachama wake. Matumizi yasiyofaa ya teknolojia hii yanaweza kusababisha vihatarishi ikiwa ni pamoja na:

a) Vihatarishi vya kimkakati vinavyotokana na maamuzi yasiyo sahihi katika uwekezaji unaohusiana na teknolojia;

b) Vihatarishi vya uendeshaji vinavyosababishwa na kutotoa huduma stahiki kutokanana kuvurugwa kwa mifumo ya teknolojia inayowezesha utoaji wa huduma kwa wanachama; na

c) Vihatarishi katika matumizi ya mifumo kutokana na uvunjaji wa taratibu zakiusalama.

5.2 Wajibu wa Bodina Menejimenti

5.2.1 Wajibu wa Bodi

Katika usimamizi wa vihatarishi vya teknolojia ya habari na mawasiliano, Bodi ya chama inapaswa kufanya yafuatayo:

a) Kupitishamkakati naseraya TEHAMA yachama;

b) Kuhakikisha kuwa mkakati wa biashara wa chama unaendana na mkakati wa TEHAMA;

c) KuhakikishakuwamuundowaTEHAMAwachamaunasaidia mwelekeo wabiashara ya chama;

d) Kutathmini utendaji wa Menejimenti katika kutekeleza mikakati yaTEHAMA, ambao unahakikisha kuwa TEHAMA Inaleta faida kwenye biashara ya chama;

e) Kuhakikisha kuwa uwekezaji wa chama katika TEHAMA una manufaa na kwambabajeti za TEHAMA zinakubalika.

f) Kufuatilianjiaambayo Menejimentiimetumiakupatarasilimaliza TEHAMAambazo zinahitajika katika kufikia malengo ya kimkakati; na

g) Kuwa na uelewa wa chama kuhusu vihatarishi vya TEHAMA na kutathmini ufanisiwa menejimenti katika ufuatiliaji na udhibiti wa vihatarishi.

CamScanner

5.2.2 Wajibu wa Menejimenti

WajibuwaMenejimentikatika usimamiziwavihatarishivyaTEHAMAni kamaifuatavyo:

a) Kuhakikisha watumishi wote wanapata Mafunzo ili wazielewe sera na taratibu za usimamizi wa vihatarishi vya TEHAMA zilizopitishwa na kuidhinishwa na Bodi;

b) Kuhakikisha kuwa taarifa za wanachama, za kifedha za bidhaa na mifumo wa kibenki zinatambulika na zinafanyika katika mazingira salama;

c) Kutoa taarifa kwa wakati kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika kuhusu matukio mabaya ya mifumo ya habari na mawasiliano au matukio yasiyotarajiwa, na jinsi ambavyo yamekuwa yakishughulikiwa;

d) Kushirikiana na Ofisi ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika katika uchunguzi wa usimamizi wa vihatarishi vya mifumo ya habari, na kuhakikisha kuwa maoni ya wasimamizi yanafuatwa; na

e) Kufanya kazi zingine yanazohusiana na usimamizi wa vihatarishi vyaTEHAMA.

5.2.3 Mkuuwa idaraya Teknolojia yaHabari na Mawasiliano

Yafuatayoni majukumuyaMkuu waidarayateknolojiayahabari na mawasiliano:

a) Kufanya maamuzi muhimu yanayohusisha matumizi ya TEHAMA kwa ajili ya maendeleo ya chama.

b) Kuhakikisha kuwa mifumo ya habari inakidhi mahitaji ya chama na mikakati ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

c) Kuratibu na kusimamia kwa ufanisi muundo wa mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano yenye ufanisi kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya chama katika teknolojia ya habari na mawasiliano. Hii ni pamoja na bajeti ya TEHAMA, usimamizi wa vihatarishi, sera, viwango na taratibu; udhibiti wa ndani wa maendeleo yakitaalam, mipango na usimamizi wa mradi wa teknolojia ya habari na mawasiliano, mfumo wa habari na urekebishaji, shughuli za teknolojia ya habari na mawasiliano, miundombinu, Usalama wa habari, mpango wa uokoaji wa janga, uhamishaji teknolojia ya habari na mawasiliano na mfumo wa taarifa za wastaafu;

d) Kuhakikishakuwakunakuweponaufanisiwausimamiziwavihatarishivyateknolojia ya habari na mawasiliano katika chama; na

e) Kuandaamafunzo yakitaalam ilikuboreshaustadiwakiufundiwa watumishi.

CS CamScanner

5.2.4 MchakatowaajirazaWatendaji

Chama kinatakiwa kuwa makini katika kuajiri watumishi, watoa huduma na wakandarasi wenye uwezo ili kupunguza vihatarishi vinavyohusiana na teknolojia ya habari na mawasiliano.

Watumishi, Watoa huduma na Wakandarasi ambao wameidhinishwa kutumia mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano za chama wanatakiwa kulinda na kutunza siri za chama.

5.3 MkakatiwaTeknolojiaya Habari na Mawasiliano

Chama kinatakiwa kuandaa mkakati wa teknolojia ya habari na mawasiliano ambao unaendana na mpango wa biashara wa chama. Chama kinapaswa kuhakikisha kuwa kuna rasilimali za kutosha (fedha na watu) zimetengwa ili kuhakikisha uthabiti na usalama katika usimamizi wateknolojia ya habari na mawasiliano.

5.4 Miundombinuya TeknolojiayaHabarinaMawasiliano

Wakati wa kuweka miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano, chama kinapaswa kuzingatia maelekezo ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

KwakuzingatiaMwongozohuu, chamakitapaswakufanya yafuatayo:

a) KuainishamajukumuyaBodinaMenejimentikatikakutekelezaseranataratibuza teknolojia ya habari na mawasiliano;

b) KuwanakitengokinachoshughulikiamasualayaTEHAMApale inapohitajika;

c) Utunzaji wataarifa zamifumo ndani nanjeyachama;

d) Utekelezajiwampango waudhibitiwa majanga;

e) Uwezowakutunzataarifazabidhaanazawanachama;

f) Kuhakikishakuwepokwamfumowenyeuwezowakutoataarifa za kisheria;

g) Matumiziyakanzidata(*database*)kwakuzingatiaviwango vyasekta husika;

h) Kuendananaviwango vyamifumo ya uendeshaji;

i) Ufikiwajiwamfumowahabari;

j) Mahitajiyataarifayauendeshaji;

k) Mahitajiyaudhibiti wa ndani;

l) Usalamawamali;

m) Uhifadhitaarifa;na

n) Utumiajiwahuduma za nje(*outsourcing*).

CamScanner

5.5 Serana TaratibuzaUsimamizi waTeknolojiaya Habari na Mawasiliano

Chama kinapaswa kuwa na sera mbalimbali madhubuti za usimamizi wa teknolojia ya habari na mawasiliano, ambazo ni pamoja na:

a) Serayausalama wa TEHAMA;

b) Serayauandaajinamajaribio ya mfumo;

c) Serayauendeshaji nauaandaajiyaTEHAMA;

d) Serayaufikiwaji naudhibiti;

e) Serayausalamawamali;

f) Serayakuwezeshamtu kutumia mfumo;

g) Serayamabadiliko yamatumiziyamfumo;

h) Serayautumishi;na

i) MpangowaBiashara na mabadilikoya Menejimenti

5.6 Utambuziwa Vihatarishi

Utambuzi wa vihatarishi unajumuisha utambuzi wa kila aina ya vihatarishi vinavyoweza kujitokeza wakati wa kuandaa mfumo wa TEHAMA ambao unaundwa na vifaa mbalimbali kama mitandao ya ndani na nje, vifaa, programu, mfumo wa muingiliano, uendeshaji na shughuli na masuala ya kibinadamu.

Vihatarishi vya usalama vinapojitokeza vinaweza kusababisha usumbufu na uharibifu ndani ya chama.

Vyanzovyotevyakihatarishilazimavibainishwenakufanyiwatathmini.Vyanzohivyoni pamoja na:

i. MajangayaAsili— mafuriko,matetemeko ya ardhi, na vimbunga;

ii. Majanga yanayosababishwa na binadamu - Hivi ni vihatarishi vinavyosababishwa na binadamu kama vile kufanya jambo kwa kukusudia au kutokusudia kama shambulio la mtandao, kusambaza virusi vya kompyuta, uchukuaji wa taarifa usioidhinishwa, na kuingiza data kwa makosa bila kukusudia; na

iii. Majanga ya kimazingira - kwa mfano, ukosefu wa nishati, uchafuzi wa mazingira, kemikali, uharibifu wa maji, n.k.

UsimamiziwavihatarishivyaTEHAMAkatikachamaunapaswakujumuishavyanzo vilivyotajwa hapo juu.

5.7 Tathmini,UpimajinaUfuatiliajiwaVihatarishi

Chama kinapaswa kuainisha na kufuatilia matukio mabaya yanayoweza kutokea siku zijazo ambayo yanaweza kuwa na athari katika mifumo ya TEHAMA na kuweka mpango wa kuyadhibiti matukio hayo.

5.7.1 Upimaji wavihatarishi

Chama hakina budi kuweka utaratibu wa kupima na kufuatilia vihatarishi kwa kufanya yafuatayo:

i. Mapitioya kabla nabaadayautekelezaji wamiradi yaTEHAMA;

ii. Ukaguziwamarakwamarawautendajiwamfumokwakuzingatiaviwango vilivyowekwa;

iii. Taarifazamatukio namalalamiko juu yahudumazaTEHAMA;

iv. Taarifazaukaguziwandani,ukaguziwanje,namasualayaliyobainishwana Tume ya Maendeleo ya Ushirika;

v. Kufanyamakubalianonawatoahudumayakupitiamikatabayahudumakwa kipindi maalum;

vi. Atharizinazowezakutokeakutokananaujio wateknolojia mpya;

vii. Kupitiakwawakativihatarishi vyauendeshaji na udhibiti wake; na

viii. Kufanya tathminiyahali yavihatarishivyateknolojiakwenye miradikupitiawatu wa nje.

5.7.2 Uzuiajiwavihatarishi

Uzuiaji wa vihatarishi unajumuisha kuweka vipaumbele, kutathmini, na kutekeleza mpango wa kupunguza vihatarishi uliopendekezwa kutokana na tathmini ya vihatarishi iliyofanyika.

Kwa kuzingatia kuwa kazi ya kuzuia vihatarishi siyo rahisi, ni jukumu la Menejimenti ya chama kuhakikisha kuwa vihatarishi vinadhibitiwa katika kiwango kinachokubalika na kwa gharama nafuu ili kuweza kulinda rasilimali za chama na kufikia malengo yaliyowekwa.

Hivyo, chama kinapaswa kutekeleza kikamilifu hatua za kupunguza vihatarishi kwa kuzingatia sera za usimamizi wa vihatarishi vya TEHAMA. Hatua hizo ni pamoja na:

a) Kuandaa ya sera za usimamizi wa vihatarishi vya TEHAMA zilizoorodheshwa wazi, viwango vya kiufundi, na taratibu za uendeshaji ambazo zinapaswa kuwekwa wazi kwa watumishi wa chama na kufanyiwa maboresho mara kwa mara;

b) Maeneo yenye mgongano wa kimasilahi yanapaswa kuainishwa na kufuatiliwa.Aidha, kunatakiwa kuwepo kwa muundo unaofaa wa udhibiti ili kuwezesha kufuatilia na kudhibiti shughuli za biashara za chama katika ngazi mbalimbali. Muundo unapaswa kujumuisha yafuatayo;

   (i) Kufanyamarejeo/maboreshokatikangazizajuu,
   (ii) Udhibiti juu yaufikiwaji naupatikanaji wadata katika mfumo,
   (iii) Idhiniiliyotolewakwaanayehusikanakiwango chachiniawali,
   (iv) Mfumo wamamlakanakutoaidhini,na
   (v) Mfumowauhakiki namalinganisho.

5.8 UdhibitinaUkaguzi wa Ndani

5.8.1 Ukaguziwandani

Kazi ya ukaguzi wa ndani wa TEHAMA inaweza kufanywa na mtu/kitengo maalumu cha ukaguzi wa TEHAMA au kufanywa na kitengo cha ukaguzi wa ndani cha chama. Majukumu ya ukaguzi wa TEHAMA ni pamoja na:

i. Kuweka na kutekeleza mpango wa ukaguzi ambao utasaidia katika kutathmini ufanisi wa mifumo ya TEHAMA ya chama na mifumo ya udhibiti wa ndani;

ii. Kutoamapendekezo kulinganana matokeo yakaziinayofanywa;

iii. Kuhakikishakuwamapendekezo yaliyotolewayanafanyiwakazi;na

iv. Kufanya ukaguzi maalum wa mfumo ya TEHAMA. Hii inajumuisha kuchunguza, kuchambua na kutoa taarifa juu ya mfumo wa TEHAMAi kutokana na taarifa ya vihatarishi itakayowasilishwa na mkaguzi wa ndani na menejimenti ya usimamizi wa vihatarishi.

5.8.2 Mawandayaukaguzi wandaniwaTEHAMA

Kwa kuzingatia aina, ukubwa na mazingira ya biashara, mifumo ya TEHAMA na tathmini ya vihatarishi vya TEHAMA, kamati ya ukaguzi/usimamizi inapaswa kuanisha mawanda na idadi ya ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA.

Ukaguziwandani wamifumoyaTEHAMA unapaswakuzingatia mamboyafuatayo:

i. Kufanyatathminiyavihatarishi vyamifumoya TEHAMA;
ii. Kufanyamapitioya serayaTEHAMA, mkakatinamwelekeo;
iii. Programuyausimamiziwamwendelezowabiashara;
iv. Mabadilikoyamifumonaudhibiti wake;
v. Utoajiwataarifa, uchambuzina ukaguziwamifumo;
vi. Jinsi ya kuingizana kutoataarifa;
vii. Ulinzi wavirusi vya kompyuta;
viii. Utoshelevuwamfumo wakitambulisho nauthibitishaji.
ix. Uendeshajinausimamizi wa mtandao.

5.8.3 Jukumu laukaguziwandanikatikautekelezajiwamfumompya

Chama kinapaswa kushirikisha kazi za ukaguzi wa ndani na usimamizi wa vihatarishi wakati wa kutengeneza na kutekelezwa kwa mfumo mpya na kuhakikisha kuwa mfumo wateknolojia ya habari na mawasiliano unakidhi viwango na unazingatia uendeshaji bora.

CamScanner

SEHEMUYASITA

UDHIBITIWAKIHATARISHICHAUKWASI

6.1 Utangulizi

Ukwasi ni hali ya chama kuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji ya chama ya muda mfupi ambayo yanatakiwa kulipwa kama vile mahitaji ya mkopo na uchukuaji wa akiba za wanachama.

Kihatarishi cha ukwasi ni hali ya chama kushindwa kutimiza au kutekeleza madai ya muda mfupi ambayo yanakuwa yameiva/tayari kwa ajili ya kulipwa. Hali hii inatokana na chama kushindwakutimiza/kukidhi mahitaji yamaombimapyayamikopo nakufanyatengolaakiba isiyotarajiwa kwa gharama ndogo. Kihatarishi cha ukwasi kwa mapato na mtaji wa chama ni pale chama kinaposhindwa kulipa dhima za muda mfupi kwa wakati, pindi zinapoiva. Ukosefu wa ukwasi chamani unaweza kusababisha chama kuwa na mtikisiko wa kifedha au kufilisika.

Ukwasi, mara nyingi unaangaliwa sana kama kihatarishi kikuu kwenye chama. Hali hii inatokea pale faida inayopatikana kutokana na mali za muda mfupi inaposhindwa kukidhi madeni ya muda mfupi.

6.2 WajibuwaBodinaMenejimentikatikakudhibitikihatarishichaUkwasi

6.2.1 Wajibu wa Bodi

KazizaBodikatikakudhibiti vihatarishivyaukwasinipamojana:

a) Kuweka kiwango cha ukomo wa ustahimilivu wa kihatarishi cha ukwasi na kuanzisha mkakati wa kudhibiti kihatarishi hicho unaoendana na mawanda ya kiutendaji wa chama husika;

b) Kuanzisha sera na taratibu za kusimamia vihatarishi vya ukwasi wa chama, ambazo zitakuwa zinafanyiwa mapitio ya mara kwa mara, angalau kila mwaka;

c) Kuteua msimamizi mwandamizi atakayewajibika, mwenye uwezo na weledi wa kusimamia vihatarishi vya ukwasi;

d) Kufanyaufuatiliajiwautendajidhidiyahalihalisiyakihatarishichaukwasi;

e) Kuhakikisha kwamba matukio ya vihatarishi vya ukwasi yanatambuliwa, yanapimwa na yanafanyiwa tathmini na kudhibitiwa;

f) Kuanzishanakufanyamapitioyaukomokatikamalizachama,muundowamtaji, ubora na ukamilifu wa mali za ukwasi, pamoja na mpango wa dharura wa fedha;

g) Kuainishamamboyanayopaswakuwepokwenyetaarifanaidadi/mudawakutoa taarifa za vihatarishi vya ukwasi itakayowasilishwa kwenye Bodi; na

h) Kutoataarifakwamamlakayausimamizikuhusumabadilikoyoyotemakubwa yanayoathiri au yatakayoathiri mpango wa sasa au wa baadaye wa ukwasi wa chama.

CamScanner

6.2.2 WajibuwaMenejimentiyachama

Chama kinatakiwa kuwa na muundo na taratibu mahususi za kufuatilia mwenendo wa kila siku na wa muda mrefu katika kusimamia na kudhibiti vihatarishi vya ukwasi kulingana na mkakati, sera na taratibu zilizothibitishwa na Bodi. Menejimenti, kwa kupitia kamatimaalumu yaudhibiti wavihatarishi vyaukwasi, itawekamfumo rahisi wakutekelezamkakati na kufanya uratibu miongoni mwa vitengo au idara nyingine. Pamoja na kazi nyingine, Menejimenti inawajibika kufanya mambo yafuatayo:

a) Kutafsiri mkakati uliothibitishwa na Bodi, malengo na kiwango cha ukomo wa kihatarishi cha ukwasi katika viwango vya utekelezaji;

b) Kufuatilia muundo wa usimamizi na udhibiti wa vihatarishi ili kuweka mikakati stahiki ya kudhibiti kihatarishi husika;

c) Kuhakikishakuwamakisioyamtiririkowafedhayanafanywabaadayamudawarobo mwaka;

d) Kutekeleza mfumo wa mawasiliano unaowezesha usimamizi wa ukwasi wa chama kwa kutambua, kupima na kufuatilia pamoja na kudhibiti vihatarishi vya ukwasi;

e) Kuweka mfumo wezeshi na imara wa udhibiti wa ndani utakaosimamia mchakato wa udhibiti wa vihatarishi vya ukwasi kwa kuainisha majukumu ya kila mmoja na kuwezesha taratibu za kukabili upungufu wa ukwasi wa chama;

f) Kuhakikisha kuwa chama kinatunza mali zake na kuwepo na ukwasi toshelezi ili kukabiliana na upungufu wa ukwasi; na

g) Kuwasiliana na Bodi kwa haraka pale kunapotokea mabadiliko makubwa ya sasa au tarajiwa ya ukwasi wa chama.

6.2.3 KamatiyaMalinaMadeni/dhimazachama

Hatari ya ukwasi huongezeka kulingana na kuongezeka kwa wigo wa shughuli za kila siku zinazofanywa za chama husika. Kwa SACCOS kubwa ni muhimu kuwa na Kamati ya Usimamizi wa mali na dhima za chama ili kuzisimamia ipasavyo. Katika usimamizi wa mali na dhima za chama, Kamati ya Usimamizi inapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

a) Kutengenezanakupendekezaserayaukwasi kwaajili yakuthibitishwanaBodi;

b) Kusimamiautekelezajinakuimarishamfumowamawasilianoambaoutasaidia kubaini, kupima, kufuatilia na kudhibiti vihatarishi vya ukwasi wa chama;

c) KuhakikishakuwamfumowautawalauliowekwanaBodikuhusukudhibitivihatarishi vya ukwasi unazingatiwa ipasavyo;

d) Kufanya mapitio mara kwa mara ya taarifa za uongozi kuhusu ukwasi wa chama; na

e) Kutoa taarifa ya kina inayohusu mfumo wa usimamizi wa ukwasi wa chama kwa Bodi angalau kwa kila robo ya mwaka.

CamScanner

6.3 SeranaTaratibuza Usimamizi

Ili kukabiliana na Hatari zitokanazo na ukosefu wa ukwasi katika chama, chama kitaanzisha sera ya usimamizi wa ukwasi inayozingatia mambo muhimu ya chama yanayoshabihiana/kuendana na sera ya mali na dhima za chama. Sera hiyo, pamoja namambo mengine, itazingatia:

i. Kubainishwa kwa majukumu na wajibu wa kila ngazi ya uongozi wa chamakulingana na muundo wa chama;

ii. Kuwepo kwa mfumo wa mawasiliano ndani ya chama ili kupata kwa wakati, taarifa zinazohusu mambo ya ukwasi wa chama;

iii. Kuruhusuuchambuziwabidhaanamuundowakenakufanyamapitioya amana za chama;

iv. Kuwekautaratibuwautambuzinaupimajiwaukwasiwachamamarakwa mara na kutoa taarifa kwenye menejimenti;

v. Kuoneshampangowaukwasishajichamaninanamnayakuepukahatariza kutokuwa na ukwasi wa kutosha chamani;

vi. Kutoa mwongozo wa kuimarisha kiwango cha chini cha ukwasi kulingana na matakwa ya mwongozo uliotolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika;

vii. Kufanya makadirio ya mtiririko wa fedha kwenye chama na kuonesha vyanzo vya fedha katika chama;

viii. Kutoautaratibumadhubuti wamatumiziyafedha yaziada (*exessliquidity*);na

ix. Kuainisha vyanzo vya fedha na kuweka kiwango kinachoruhusiwa cha fedha kutoka nje ya chama, na kiwango hicho ni lazima kipate idhini.

6.4 Upimajiwa Vihatarishivya Ukwasi

Ili kiweze kutambua mipaka na hali halisi ya ukwasi Chama hakina budi kiwe na viashiria vinavyoonesha kiwango halisi cha ukwasi wa chama. Hivyo, chama kitatakiwa kuwa na vipimo vya ukwasi kwa lengo la kubaini hali halisi ya ukwasi wa chama kwa muda husika na kuchukua hatua stahiki ya kuimarisha ukwasi unaohitajika pale kutakapokuwa na upungufu.

6.4.1 Takwalakisherialakiwangochachinichaukwasiwa chama

Kiwango cha ukwasi wa chama kitazingatia Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo ya fedha ili kulingana na takwa la kisheria. Kwa sasa, sheria inakitaka chama kuwa na ukwasi wa mali usiopungua 15% ya Amana, na dhima za muda mfupi katika mali za ukwasi.

6.4.2 Uwianomwinginewa ukwasi

Chama kinatakiwa kutumia uwiano tofauti tofauti katika kupima hali halisi ya ukwasi na kutathmini mwelekeo wa chama. Baadhi ya uwiano unaotumika kupima ni kama ifuatavyo:

CamScanner

a) **Uwianounaohusumaliza chama (*Asset based ratio*)ni pamoja na;**

i. Kiashiriachahali yafedhaTaslimu; na

ii. Uwianowauwezowamalikuzalisha(*CapacityRatio*)

b) **Uwianowadhimaza chama(*Liability-basedliquidity measures*)**

i. UwianowaJumlawaAmana(*Total deposit ratio*);

ii. Uwianowafedhayaununuzi(Purchased funds ratio); na

iii. Uwianohalisiwaamana (Coredeposit ratio).

c) **Uwianowa mali nadhima (*Asset and Liquidityratio*)**

i. Uwianowamikopo naamana(*loan to deposit ratio*)

ii. UwianousiohalisiwautegemeziwamfukoNetnon-corefunding dependence ratio

6.5 Ufuatiliajiwa ukwasi(*Liquidity Monitoring*)

Chama kitakuwa na mfumo utakaowezesha kupima, kufuatilia, kuthibiti na kutoa taarifa za vihatarishi vya ukwasi katika hali ya kawaida na isiyo ya kawaida ya kiutendaji. Mfumo huo utajumuisha taarifa zote kuhusu visababishi vya hatari katika ukwasi kutokana na shughuli za kibiashara za chama, pamoja na uanzishaji wa bidhaa mpya katika chama. Mfumo utakuwanauwezo wakufanyatathminiyavisababishi nakupimaatharizakekatika mtiririkowafedha na hali ya uwiano wa ukwasi wa Chama.

6.6 MpangowaDharurawaUkwasi(*LiquidityContingencyPlanning*)

6.6.1 Utangulizi

Chama kitaandaa mpango wa dharura wa ukwasi ambao utaweka mkakati wa kukabiliana na mtikisiko wa ukwasi na taratibu zitakazowezesha kusaidia mpango wa dharura katika kukabiliana na hali ya mtiririko hasi wa fedha. Mpango huo utasaidia chama kubaini na kuelewa aina ya matukio ambayo yanaweza kuathiri mpango wa dharura wa ukwasi katika chama.

Mpangowadharurautakuwaunafanyiwa mapitio yamarakwamara(angalau maramojakwa mwaka) na Menejimenti au kamati ya usimamizi wa vihatarishi ili uendelee kuwa imara na kutekelezeka wakati wote. Chama kitafanya majaribio ya mara kwa mara ya mpango wa dharura ili kuweza kujiandaa na mambo yasiyo tarajiwa.

6.6.2 Viashiriavyamapemavya tahadhari

Ili kupima iwapo kuna tatizo la ukwasi katika chama, na kuwezesha kuwa na mpango wa udhibiti, chama kitakuwa na viashiria vya ndani na vya kimasoko ikiwa ni pamoja na:

(a) Viashiria vya Ndani

i. Kuharibikaau kushukakwaubora wamali(Deteriorating asset quality);

CamScanner

ii. Utegemeziuliopitilizakwamalimojanachanzokimojachafedha;

iii. Kushukakwamapato naribatarajiwa;

iv. Kuongezekakwagharamazafedha/kupatafedha;

v. Ukuajiwaharakawamikoponamalizakudumuambazozinatokananagharama kubwa za mikopo na amana katika chama; na

vi. Mtiririkowafedhausioridhishaunaofanyakutokuweponamlinganishowa mapato na matumizi hasa kwa kipindi kifupi.

(b) Viashiria vya masoko

i. Gharamakubwazakupatamikopo yanje;

ii. Kupunguakwawatoahuduma zakifedha;

iii. Mwitikio mdogo wa wawekezaji wa muda mrefu na watoa mikopo isiyokuwa na kinga kwa chama; na

iv. Kuongezekakwauchukuaji waamanazawanachama.

Chamakinatakiwakuwa namfumowakubainnakufuatiliaviashiriahivi ilikuwezakukabili au kudhibiti mapema iwezekanavyo, matatizo yanayoweza kujitokeza.

6.6.3 MkakatinaTaratibu(*Strategyand Procedures*)

Mpangowadharurawaukwasikwaajiliyakukabilivihatarishivyaukwasiutazingatia mambo yafuatayo:

a) **Ushirikiano wa kiutawala** – Taratibu za kutoa taarifa zitaanzishwa ambapo taarifa muhimu kuhusu utekelezaji wa mpango huu zitawasilishwa kwenye Menejimenti au kamati ya mpango wa dharura kwa ajili ya kufanya maamuzi ya haraka. Mfumo huu utaainisha majukumu na wajibu wa kila mtu katika utekelezaji hasa wakati wa dharura;

b) **Viashiria vya onyo la mapema** - Chama kitaweka mazingira ya kupata viashiria vya onyo ya kihatarishi mapema ili kuweza kubaini namna nzuri ya kukabiliana na tatizo na kuwezesha upimaji, ufuatiliaji na utoaji wa taarifa wa viashiriahivyo;

